# GUNDUA MTANDAO WAKO

MADA YA

4

***Alama ya Chapisho***

Februari 2022

Programu ya ‘Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?’ linaweza kuwa huru kutumika, kwa vile chanzo kimetajwa.

***Ilianzishwa na:*** Wil Bom, VSO, mradi wa Vijana na Ajira, Zanzibar, Tanzania

***Kwa ushirikiano na:*** Walimu na wakufunzi wasaidizi wa makundi manne ya Mafunzo ya Ufundi (Amali), Unguja na Pemba; Sophie Oonk wa Randstad Uholanzi ambaye aliendeleza mada ya 5 ‘Gundua biashara yako’; Kitty den Boogert, rafiki na mwenzangu wa zamani, ambaye aliangalia toleo la mwisho.

***Kwa kuzingatia:*** Warsha (ya mafunzo) ya maendeleo ya kazi, iliyotolewa wakati wa maonesho ya Zanzi Job ya mwaka 2015 na 2016.

Utangulizi wa VSO-ICS juu ya uajiri na ujuzi wa maendeleo ya kazi katika mwaka 2015 na warsha (za mafunzo) zilizotolewa na Watu wenye Kujitolea wa Huduma za Wananchi, Kimataifa.

Mwongozo wa mafunzo, Elimu ya Ujasiriamali na Mafunzo ya EET, Kuboresha Uwezeshaji wa Kiujasiriamali, Moduli ya 1 na 2, VETA, 2014 – 2008.

Maendeleo ya programu kwa mwongozo wa kazi katika mafunzo ya ufundi na CINOP, Uholanzi. www.cinop.nl

Loopbaanmagazijn (Hifadhi ya kazi), ilianzishwa na Claudine Hogenboom, mradi wa Mwongozo wa Kazi kwa mafunzo ya ufundi, Uholanzi. http://www.expertisepuntlob.nl/

Het lespakket netwerken (Mtandao wa Mtaala), ilianzishwa na La Red B.V., Uholanzi. http://lared.nl/

***Tafsiri ya Kiswahili:*** Abdalla Baruan, Dar es Salaam, abbybaruan@gmail.com
Abraham Mtongole, Dodoma, abmtongole@gmail.com
Yahya Abdu, Pemba, Tafsiri ya kiswahili na uhakiki wa toleo la mwisho, yahyarashid@live.com

***Ubunifu:*** Katie Wolgemuth, VSO Dar es Salaam na wanafunzi wa GLU, Grafisch Lyceum Utrecht

***Ilichapishwa na:*** VSO Tanzania, S.L.P 6297, Dar es Salaam Tanzania

***Eneo:*** Ploti na. 997 Msasani, Barabara ya Chole, Dar es Salaam Tanzania

***Simu:*** (+255) 222600072 au (+255) 222600087


***Barua pepe:*** vsotanzania@vsoint.org

***Tovuti:*** www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet




# MAENDELEO YA KAZI NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?

## MADA YA 4 GUNDUA MTANDAO WAKO



# YALIYOMO

Kitabu hiki 'Gundua mtandao wako' ina vifaa kwa ajili ya mada ya 4 ya programu kwenye Maendeleo ya Kazi. Kwanza, unakuta utangulizi wa jumla kwenye programu na namna ya kuandaa mafunzo. Hii inafuatiwa na maelezo mahsusi ya jumla ya mazoezi ya mada ya 4, maelekezo tofauti kwa kila zoezi na karatasi za mazoezi.


| | |
|---|---|
| Utangulizi wa jumla Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi naa jira au ajira binafsi? | 6 - 11 |
| Mada ya 4 na maelezo ya jumla ya mazoezi 'Gundua mtandao wako' | 12 - 15 |
| Mada ya 4: mazoezi 4.1 - 4.21 | 16 - 57 |
| Karatasi za mazoezi | 58 - 99 |


Vichwa vya vitabu vyote sita vya programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi? ni:

1 Gundua kipaji chako
2 Gundua shauku yako
3 Gundua ulimwengu wako wa kazi
4 Gundua mtandao wako
5 Gundua biashara yako
6 Mpango kazi wako na kuomba kazi

Uwasilishaji wa pawapointi na karatasi za mazoezi zinaweza kupakuliwa kutoka www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

# UTANGULIZI WA JUMLA

# MAENDELEO YA KAZI: NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?

**Mradi wa VNA na programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi'**
Vijana na Ajira (VNA), mradi wa Vijana na Ajira ni moja ya miradi ya VSO, Volunteer Services Oversee (Huduma za Kujitolea, Ng'ambo) kwa ushirikiano na RGZ, (Revolutionary Government of Zanzibar/Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar). Moja ya vipengele vya mradi wa VNA ni programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi' (UWwK).


Programu ya UWwK hutaka kuimarisha nafasi ya kijamii na kiuchumi ya vijana ndani ya Zanzibar kwa kuendeleza ustadi mbalimbali wanaouhitaji kwa ajili ya ajira, ajira binafsi au ujasiriamali. Kwa kusudio hilo, viunganishi madhubuti zaidi baina ya sekta binafsi na mafunzo ya ufundi ni muhimu. Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi (Amali) (MMA), NACTE (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi), Vituo vyote vya Mafunzo ya Ufundi (Amali) na Taasisi za Zanzibar zinahusishwa kama washirika katika programu hii ya UWwk. Wana majukumu makubwa katika kuwawezesha vijana pamoja na ujuzi muhimu kuingia katika soko la ajira.

Programu ya UWwK imezalisha sanduku la zana kwa masomo mawili ya msingi: Mafunzo na Elimu ya Kuzingatia Umahiri na Maendeleo ya Kazi. Unaweza kupata sanduku zima la zana kwenye mtandao: www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

**Maendeleo ya Kazi**
Programu ya 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' ikiwemo uchaguzi mpana wa mazoezi ya darasani ambayo husaidia wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi kupata kuonekana zaidi katika mazingira ya kazi. Kwa kufanya kazi, wote, wale wa ndani ya darasa na nje katika mazingira halisi, vijana hupata habari za hapo kwa hapo kuhusu ulimwengu wa kazi, hufanya kwa vitendo ujuzi tofauti wanaouhitaji kwa ajili ya maendeleo yao ya kazi na hubadilishana uzoefu kwa kila mmoja kati yao. Vipindi vitabuniwa na kutolewa na VMA (Vituo vya Mafunzo ya Amali), Taasisi za Ufundi, Skuli za Sekondari na mashirika mengine ya kiserikali na yasio ya kiserikali, kawaida ni kwa mchango wa wafanya biashara wa ndani (wenyeji). Waajiri na kiongozi (meneja) wa rasilimali watu anaweza kuwa msaada kwa kuwezesha safari za kimasomo, kwa kuwa mkufunzi mgeni wa ndani ya madarasa au kwa kutoa mafunzo ya viwandani.

**Programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?**
Programu ya Maendeleo ya Kazi huwawezesha walimu wa skuli za sekondari, wakufunzi wa taasisi za mafunzo ya ufundi, kampuni, taasisi zisizo za kirerikali, wizara ya Kazi, Ajira, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Amali) kuchagua mazoezi ambayo yanafaa kwa mahitaji na kiwango cha makundi yao ya vijana.

Programu hailengi kwa vijana kufanyia kazi kwa kujitegemea, bila mwongozo wowote. Bila shaka, washiriki hupata kazi au kazi fulani ya kufanya mmoja mmoja, lakini kwa jumla, hii ni programu ambayo inahitaji mwingiliano, ushirikiano katika makundi na mrejesho. Haiwezi kufuatwa bila mwongozo. Hakikisha unatoa daftari ambalo washiriki wanaweza kuandika na kuhifadhi matokeo na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka mwelekeo wa kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wa mbele. Walimu na wakufunzi wanahitaji kujiandaa vizuri, na inapendekezwa kwamba mwanzo watafakari maendeleo yao wenyewe ya kazi. Kwa njia hii, walimu na wakufunzi pia ni mfano wa kuigwa katika kuendesha kazi yao wenyewe kiundani.




**Mahiri sita za kazi na dira ya kazi**
Programu 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' imeundwa karibu na mahiri sita ambazo ni muhimu wakati unapotaka kuendeleza kazi yako:

1 Gundua kipaji chako: tafakuri kuhusu uwezo, kupitia umahiri wako mwenyewe kwa heshma ya kazi yako;

2 Gundua shauku yako: tafakuri kuhusu hamasa, kupitia matakwa na maadili yako mwenyewe kwa heshima ya kazi yako;

3 Gundua ulimwengu wako wa kazi: utafutaji wa ajira, mwelekeo kuhusu maadili na umahiri wako kulinganisha na kinachohitajika katika hali ya kazi za kitaaluma;

4 Gundua mtandao wako: mtandao, kufanya na kudumisha mawasiliano ambayo ni muhimu kwa kazi yako;

5 Gundua biashara yako: utafutaji wa ajira binafsi, mwelekeo juu ya matarajio na umahiri wako kuanza biashara au kuendeleza kazi kama mjasiriamali;

6 Mpango kazi wako na kuomba kazi: udhibiti wa kazi, mipango inayohusiana na kazi na ufafanuzi binafsi wa nafasi kwa mchakato wako wa kujifunza na kazi.

Kila umahiri wa kazi umeshikamanishwa sambamba na swala la kazi na jumla ya mahiri sita zinawakilishwa kama usukani wa uendeshaji wa kazi. Unahitaji kuendesha hatua zako za kazi muda wote kutafuta mwelekeo sahihi. Katika maelezo ya kina ya kila moja ya mahiri sita za kazi, unaweza kupata ufafanuzi zaidi kuhusu umahiri unaouhitaji kufanya kwa vitendo, kuendeleza kazi.

**Namna ya kutumia programu kwenye Maendeleo ya Kazi?**
Kila umahiri wa kazi unaweza kufunzwa kwa kufanya mazoezi kadhaa. Mazoezi hutofautiana katika maudhui na katika mbinu pia. Hii ni nzuri, kwa kuwa kuna njia zaidi ya moja ya kujifunza umahiri wa kazi.

Mwanzoni mwa kila mada mpya, utakuta maelezo ya jumla ya mazoezi yote ambayo ni ya mada maalum. Katika maelezo hayo ya jumla, kawaida unakuta: jina (kichwa) cha zoezi, lengo na muhtasari wa mbinu chochezi ambazo zinaweza kutumika katika zoezi hili. Kwa njia hii, unaweza kuangalia kwa haraka mazoezi yote na hii itakusaidia kufanya uchaguzi unaokufaa na kundi lako. Uchaguzi mzuri ni ule unaohusiana na maswala ya maendeleo ya kazi ambao wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanao.

Baada ya kuchunguza maelezo ya jumla, unaweza kuvuta mazoezi uliyochangua. Yote kati yao yana muundo sawa. Kwa njia hii, unaweza kuona kwa urahisi namna ya kuandaa na kutoa zoezi kwa njia inayofaa.

Kwa kufanya uteuzi wako mwenyewe, walimu na wakufunzi wanaweza kubuni programu ya mafunzo. Unachagua mazoezi yale ambayo yanafaa kwa mtaala, ratiba ya vipindi vya kozi na kiwango cha wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi. Uchaguzi unaofanya pia hutegemea na maswali ambayo wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanayo kuhusu kazi yao.

Walimu na wakufunzi wanaweza pia kuchagua yale mazoezi wanayopenda kusomeshea. Baadhi ya mazoezi na mbinu zitakufaa zaidi kuliko nyengine. Vidokezo vinavyotolewa mwishoni mwa maelekezo, ni mapendekezo ili kuwezesha zoezi liwe vizuri iwezekanavyo, lakini jisikie huru kulifanya kwa njia tofauti unazodhani zitakufaa au vizuri zaidi kwa kundi lako.

Bila shaka, unaweza kuongeza mazoezi yako mwenyewe kwenye programu hii. Kwa njia hii, sanduku la zana litakua na kwa kubadilishana mazoezi na wengine, mwongozo wa kazi utatolewa kwa njia nzuri zaidi kwa vijana wa Zanzibar na Tanzania.

**Muundo sawa katika mazoezi yote**
Mazoezi yote yanaelezwa kwa kina zaidi, kufuata muundo huo huo. Hii itakusaidia kuandaa na kuwezesha mazoezi uliyoyachagua. Muundo ni:

**Lengo:** Ni lipi madhumuni ya zoezi? Matokeo gani yatakuwa yanatarajiwa. Kuangalia ufahamu, tabia, ujuzi na vitendo?

**Maandalizi:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini cha kufanya katika maendeleo ya kazi kwa ajili ya kutoa zoezi kwa namna ya kuzingatia mchakato? Jinsi ya kuandaa darasa kuwapa washiriki wako eneo wanalohitaji ili kufanya mazoezi? Baadhi ya mazoezi yanahitaji eneo zaidi au mpangilio tofauti wa viti/meza.

**Maelezo:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini unaweza kuwaambia wanafunzi/watafutaji wa kazi wako na wabunifu wa kazi kama ni utangulizi kwenye zoezi?

**Utendaji:** Ni nini wanafunzi/watafutaji wa kazi na watoaji wa kazi watalazimika kufanya au kuonesha katika zoezi hilo? Hapa, unaweza kupata mlolongo wa hatua ambazo washiriki huchukua ili kukamilisha zoezi.

**Tafakuri:** Mwaswali gani unauliza mwishoni mwa zoezi (au baada ya hatua mahsusi wakati wa zoezi)?

**Dondoo:** Vitu ambavyo unahitaji kuwa na uelewa navyo wakati wa zoezi.

**Uchunguzi wa kina:** Nini kinaweza kufanywa zaidi kulipa zoezi (kwenda) kina zaidi au kuliunganisha na zoezi jengine?

**Karatasi za mazoezi:** Misaada ya kujifunza, malighafi na vifaa ambavyo vinaweza kutumika na wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi.

# MADA YA 4

**Gundua mtandao wako**

Katika mada ya 4 utakuta mazoezi 21 kuhusu umahiri wa kazi 'Gundua mtandao wako': mtandao.

Gundua mtandao wako inamaanisha: kutambua mtandao wako, kuujenga na kuudumisha, hivyo unaweza kuendeleza kazi yako kwa njia nzuri iwezekanavyo. Wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi huendeleza ujuzi kutumia mtandao wao kwa namna ambayo mwanzoni kabisa wanaweza kupata sehemu katika soko la ajira na kwa baadae wanaweza kuudumisha au kuubadilisha. Hujifunza namna ya kuwasiliana kuhusu wakitakacho na wanachohitaji kwa ajili ya kazi yao.

Katika maelezo ya jumla ya mada ya 4 unaweza kuwa na uelewa mtandao ni nini na kuwatambulisha watu mtandao wako mwenyewe; kuchunguza thamani ya mtandao wako ni nini, namna ya kutoa na kupata uungwaji mkono kutoka katika mtandao wako; kuwa na uelewa na ujuzi wako wa mawasiliano na ni zipi athari za mawasiliano; kujenga, kutumia na kudumisha mtandao wako.

Nambari ambayo zoezi hilo linaendana na idadi ya maelezo ya kina ya zoezi hilo na ya karatasi za zoezi. Karatasi za zoezi zinaweza kunakiliwa kwa urahisi kwa ajili ya vijana wako. Hakikisha unatoa daftari ambapo washiriki wanaweza kuandika matokeo yao na wanaweza kuhifadhi matokea na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka dira ya kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wenyewe wa mbele.



# MAELEZO YA JUMLA YA MAZOEZI 'GUNDUA MTANDAO WAKO'

| Mazoezi 'Gundua mtandao wako' | Lengo la zoezi | Mbinu shirikishi |
|---|---|---|
| **4.1 Mtandao wa kundi letu** | Vijana wapate uelewa kwa namna ya kimchezo. Wagundue mtandao wao na namna gani wanavyohusiana. | Kwa kurusha mpira uliotengenezwa kwa sufu au kamba kwa kila mmoja, washiriki watengeneze mtandao wa kikundi chao. Itawasaidia kuona ni namna gani wanaweza kutengeneza ramani ya mtandao binafsi baadaye. |
| **4.2 Majadiliano ya kimya kwenye ukuta** | Vijana waunde maana ya dhana ya 'uundaji mtandao'. | Kwanza, kijana ajibu mwenyewe maswali mawili kuhususiana na kundi alilomo. Baadae, wachemshe bongo (bila kusema chochote) kuhusu dhana ya 'uundaji mtandao' kwa kuandika mawazo yao kwenye karatasi. Kisha katika makundi ya watu watatu watengeneze maana na hatimaye kundi zima wawe na maana ya pamoja kuhusu 'uundaji mtandao'. |
| **4.3 Je, mtandao wangu unaonekanaje?** | Vijana watoe taswira ya mtandao wao na wajue mtandao wao unavyoweza kuwa mkubwa. | Vijana watengeneze mchoro akilini na makundi tofauti ya watu wanaowajua. Wawasilishe mitandao yao katika makundi madogo kulijadili. |
| **4.4 Picha ya mtandao wangu** | Vijana watengeneze mchoro wa mtandao wao na wajue mtandao wao wajifunze kuufafanua. | Vijana wawaweke watu wanaowajua katika makundi tofauti. Baada ya hapo, watengeneze mchoro wa mtandao wao. Baadaye watafakari wenyewe juu ya michoro yao, waipitie na wajibu maswali kadhaa. Mwisho, katika makundi watafakari michoro yao na waelezee mtandao wao. |
| **4.5 Uhusiano wangu na watu ninaowafahamu una nguvu kiasi gani?** | Vijana wafikirie vile mtandao wao unavyoonekana: watu wanaowajua, wanachokifanya, kwa kiasi gani wanawafahamu, na jinsi wanavyohusiana. | Baada ya mazungumzo na ufafanuzi kuhusu ubora na udhaifu wa mtandao kati ya watu, vijana waorodheshe watu wanaowajua na kazi zao. Waoneshe uimara wa mahusiano yao. Baada ya hapo waandike majina yote katika duara na wachore mistari kati ya watu wanaojuana kuonesha nani anahusiana na nani. Hivyo, mtandao wao uonekane. |
| **4.6 Kufafana na kutofautiana kwa mtandao wangu** | Vijana wachunguze kufanana na kutofautiana kati ya washirika wa mtandao wao. Kwa vipi mtandao wao unatofautiana. | Baada ya chemsha bongo kadhaa vijana wajaze katika azimio wakiwa na watu kumi katika mtandao wao na waandike namna mbili za mfanano na tofauti mbili kati yao. Katika jozi, watafakari orodha yao na watoe baadhi ya hitimisho kuhusu kutofautiana kwa mtandao wao. |
| **4.7 Ni fani zipi zinajitokeza katika mtandao wangu?** | Vijana watengeneze ramani ya mtandao wao kwa kutaja fani kwa watu wanaowafahamu. Wanapata uelewa mzuri kwa namna gani watu tofauti kwenye mtandao wao wanavyoweza kuwa wa manufaa kwao. | Vijana wajaze orodha yenye majina na ujuzi wa watu 30. Katika kundi la watu wanne watafakari kuhusu mtandao wao na waongeze katika orodha yao watu wawili wanaowasiliana waliopendekezwa na wengine. Baada ya kujadiliana na kulinganisha orodha ya kila mmoja, vijana wachague watu wawili wanaoweza kuwaomba msaada. |

| | | |
|---|---|---|
| **4.8**<br>**Msaada wangu kwa wengine** | Vijana watafakari msaada ambao wamewapa wengine mwezi uliopita. Wajenge sifa zao na uzoefu ambao unaweza kutumika kusaidia wengine siku zijazo. | Baada ya chemsha bongo kadhaa au mazungumzo kuhusu mawazo ya 'kutoa na kupata msaada' na 'sheria ya upevukaji' vijana wajadili msaada walioutoa karibuni. Baada ya hapo waandike msaada wanaoweza kuutoa kwa wakati ujao, kwa kuzingatia uelewa wao, ubora na mawasiliano yanayotumika waliyonayo wakati wa tafakuri katika kundi zima vijana waorodheshe watu wanaoweza kuwaomba baadhi ya misaada kuhusiana na ukuzaji wa fani zao. |
| **4.9**<br>**Ni msaada gani naweza kuutumia?** | Vijana wajifunze kuunda maswali ya wazi na thabiti kwa msaada kuhusu maendeleo yao ya kazi zao. | Kwanza, wachemshe bongo kuhusu vigezo kwa usahihi na uthabiti wa maswali, kwa pamoja watengeneze orodha. Kwa kujitegemea watunge maswali yenye uhalisia kwa msaada, katika jozi maboresho kadhaa na baada ya hapo watafute katika mtandao wao nani anaweza kuwa msaada. Kama kazi ya nyumbani, wapate kazi ya kuuliza maswali hayo kwa watu walio wachagua na kuwasilisha majibu. |
| **4.10**<br>**Mawasiliano: unaweza kujifunza hili?** | Vijana wajifunze kuhusu umuhimu wa mawasiliano mazuri na yanaweza kuleta athari gani katika mahusiano yao na wengine. | Kila mshiriki atafakari juu ya kauli kadhaa kuhusu namna yake ya kuwasiliana. Katika kundi la wanne, waongee kuhusu majibu yao kwa kauli hizo. Baada ya hapo kila mshiriki afanye hitimisho kuhusu anachoweza zaidi katika mawasiliano yake na kilicho kigumu kwake. |
| **4.11**<br>**Sentensi za mwanzo: utangulizi mzuri ni nusu ya pambano** | Vijana wafikiri kuhusu sentensi za mwanzo wanazoweza kuzitumia katika hali ambazo wanapata ugumu kujitambulisha kwa watu wasiowafahamu. Wajifunze kwamba ni muhimu kujiandaa vizuri. | Kwa pamoja vijana wataje baadhi ya mazingira ambayo wanayaona kwamba vigumu kuanzisha majadiliano. Waandike sentensi za ufunguzi kwenye kipande cha karatasi, kikunje na kiweke kwenye kapu. Baaadaye karatasi isomwe kwa sauti moja baada ya nyingine na washiriki watatu watoe mrejesho wao. Sentensi zote zenye ufunguzi mzuri ziwekwe kwenye orodha. |
| **4.12**<br>**Ni nani ananivutia?** | Vijana wachunguze ni watu gani wanavutiwa nao au wanawapenda. Lengo la kushirikiana pia ni kusikiliza kwa umakini na kutengeneza muhtasari fasaha. | Vijana waandike ni watu gani anapendezwa nao na kwanini. Wafikirie wanachotaka kujifunza kutoka kwa watu hawa. Katika kundi la watatu washirikishe shukrani zao. Wakati wa kufanya kazi kwenye vikundi vidogo, wafanyie mazoezi ujuzi wa mawasiliano pia: kusikiliza kwa makini na kufupisha kwa usahihi. |
| **4.13**<br>**Ehhh, ni mimi ehhh...!** | Vijana wachunguze namna ya kuwa na mawasiliano na mtu ambaye hawamjui na namna ya kuanza mazungumzo. Wataibua 'ya kufanya' na 'ya kutofanya'. | Kwanza, jozi mbili zifanye zoezi mbele ya darasa. Baada ya tafakuri na mrejesho wa mazoezi yote, washiriki wote wapate nafasi. Wanafanya kazi katika makundi ya watu watatu: Watazamaji na wawili ambao watakuwa na majadiliano. Kila baada ya majadiliano, wabadilishe majukumu. Wakati wa kupitia katika kundi zima vijana wabaini 'ya kufanya' na 'kutofanya' orodha. |
| **4.14**<br>**Mwanamtandao halisi** | Vijana wachunguze majukumu ya mwanamtandao bora na kupima kazi zao wenyewe zihusianazo na uundaji wa mtandao. | Vijana waangalie kazi za mwanamtandao bora wanayemfahamu, watengeneze orodha yao wenyewe ya kazi za mtandao, watathmini kile wakipendacho/wasichopenda kufanya na kupima. Katika mwingiliano wa watu kijozi na kundi zima wanashirikishana upimaji wao walioufanya. |
| **4.15**<br>**Na kisha kukawa na ukimya...** | Vijana wachunguze mazingira ambamo walikwama kwenye mazungumzo. Wanafanya mazoezi ya namna ya kuendeleza mazungumzo kwa lengo la kutengeneza mahusiano ya kimtandao. | Katika jozi, vijana watafakari na kuzungumza kuhusu kujihusisha kwenye mazungumzo. Kipi kina msaada, kipi kinasumbua? Baada ya kujadili baadhi ya nadharia kuhusu mazungumzo endelevu, washiriki wawili wafanye zoezi mbele ya darasa. Baada ya tafakuri ya mfano huu, kila mmoja afanye, katika kundi la watu watatu. Mwishoni vijana wafupishe katika kundi zima walichojifunza na kutoa michango yao kwa baadhi ya sheria kuhusika kikamilifu kwenye majadiliamo. |
| **4.16**<br>**Kuwakutanisha watu wawili pamoja** | Vijana waendeleze mbinu na kufanyia zoezi ya namna ya watu wawili kutambulishana wao kwa wao. Waunde karatasi ya zoezi kwa hatua na vidokezo. Wafanyie zoezi mbinu. | Katika makundi, vijana wajibu maswali matatu kwenye karatasi kubwaza chati mgeuzo. Katika kundi zima, wafanyie kazi njia/mbinu za namna ya kutambulishana watu wawili wao kwa wao. Kwa pamoja watengeneze rasimu ya karatasi ya kazi ya mbinu hizo. Kisha washiriki watatu waigize mbele ya darasa. Watafakari juu ya hilo kwenye kundi zima na waangalie iwapo kuna marekebisho ya kufanya katika karatasi ya kazi. |
| **4.17**<br>**Je, mtandao wangu wa 'Ulimwengu wa Kazi' unaonekanaje?** | Vijana watoe hisia za mtandao wao wa 'Ulimwengu wa Kazi' na kuwa na ufahamu wa jinsi mtandao wao unavyokua au unavyoweza kukua. | Vijana watengeneze taswira ya mtandao wao kwenye karatasi kubwa. Wanawasilishe na kuelezea kwa kila mmoja na wajadiliane jinsi wanavyoweza kuufanya mtandao wao wa 'Ulimwengu wa Kazi' kuwa mkubwa. |
| **4.18**<br>**Jinsi ninavyoutumi a mtandao wangu wa 'Ulimwengu wa Kazi'.** | Vijana wachunguze kile ambacho mtandao wao unaweza kuwafanyia. Wapange shughuli muhimu ili kupata msaada wanaotaka. | Kila mshiriki ajitengenezee malengo dhahiri na madhubuti anayotaka kusaidiwa. Katika makundi, waboreshe utengenezaji wa malengo. Kisha waandike malengo hayo katika mduara kwenye karatasi kubwa au A3 na waandike katika mduara huo watu walio katika mtandao wao wanaoweza kuwa na msaada. Waandike kazi ambazo wanataka kufanya ili kupata huo msaada. Mwishoni wabuni kazi mbili za mtandao kwa ajili ya wiki ijayo. |
| **4.19**<br>**Orodha ya matakwa ya mtandao wangu wa 'Ulimwengu wa Kazi'** | Vijana watengeneze orodha ya matakwa kuhusu kile wanachotaka kufikia kuhusiana na kazi yao kwa kutumia mtandao wao wa 'Ulimwengu wa Kazi'. Wapange shughuli ili kupata msaada wanaotaka. | Kwanza vijana 'wazungumze' wajadiliane katika jozi kuhusu matakwa yao. Kisha waandike maswali 3 wanayotaka kuwauliza watu kwenye mtandao wao wa mafunzo ya viwandani au kiwandani. Katika kundi la watu wanne wajadiliane matakwa yao na namna ya kuyatimiza. Wafanye nini kupata msaada? Katika wiki 2 zijazo, wachukue hatua kuomba msaada wanaoutaka. Kwenye kipindi kinachofuata, watafakari juu ya matokeo. |
| **4.20**<br>**Kasi ya mahusiano: azungumzo na wenza wa shule nisiowajua** | Vijana wawe na mazungumzo na wenzao ambao hawawajui.. | Vijana wanaongea na wenzao kutoka kozi tofauti kuhusu masomo wanayoyasoma. |
| **4.21**<br>**Kasi ya mahusiano: mazungumzo machache na watu nisiowajua** | Vijana wajifunze wenyewe katika kuzungumza na watu ambao hawajui bila kuamua kabla juu ya mada itakayozungumziwa. | Vijana waeleze katika salamu na maongezi mafupi taratibu (kaida) za Tanzania, wawaangalie kwa kutumia orodha ya dondoo. Wachague upande upi wanataka kujaribu katika majadiliano yao pamoja na watu wengine wengi wasiojulikana katika maduka, masoko au katika mitaa wakati wa wiki mbili zijazo. |

# 4.1 MTANDAO WA KUNDI LETU

**Lengo**
Vijana wapate uelewa kwa namna ya kimchezo. Wagundue mtandao wao na namna gani wanavyohusiana.

**Maandalizi**
Hakikisha una mpira mkubwa wa sufu au kamba. Fikiria mwenyewe kama kufanya zoezi kwa namna hii au unataka kutumia baadhi ya dondoo? Weka meza na viti vyote pembezoni mwa darasa. Waombe washiriki wakusaidie.

**Maelezo**
'Katika mazingira ya kukuza fani, ni muhimu kuutazama mtandao wako. Picha yake dhahiri, inakupa fursa ya kuchukua njia ya haraka na ya muda mfupi ya kuwasiliana na watu sahihi ambao wanaweza kukusaidia kufikia malengo yako. Pamoja, tutachora mtandao kati ya washiriki wa kikundi chetu: ni jinsi gani sisi katika kikundi hiki tunahusiana? Hii itatuonesha jinsi tunavyoweza kuteka mtandao wetu binafsi wa fani baadaye. Hili ni zoezi la kupasha mwili tu.'

**Utendaji**
1. Weka meza zote na viti pembeni na waalike washiriki wote kusimama katika nafasi wazi.
2. Wambie watembee kwa kuzunguka katika darasa kwa kuchanganyana.
3. Sema 'acha' wakati washiriki wote wamesambaa vizuri katika chumba kizima. Vijana wataendelea kuwa mahali waliposimama.
4. Mpe mmoja wao mpira wa pamba (au kamba) na maelekezo ya kurusha mpira kwa mtu mwingine wakati akiwa ameshika kamba ya mpira wa pamba. Mruhusu aseme jina la mtu huyo na wakati huo huo wanaelezea uhusiano wao. Kwa mapendekezo zaidi ya mahusiano iwezekanavyo, angalia vidokezo.
5. Mshiriki ambaye anachukua mpira anaendelea kwenye uzi na airushe mipira mingine ya pamba (au kamba) kwa kusema jina na uunganisho.
6. Endelea kufanya hivyo mpaka washiriki wote wakamate kwenye uzi na mtandao wa buibui (mtandao wa mahusiano) umeundwa.
7. Chukua picha ya mtandao huu kwa simu ya mkononi na itume hii kwa washiriki wako wa kundi la whatsapp ili waweze kuiweka katika madaftari yao 'Kazi yangu'.
8. Waache watu wa mwisho kutupa mpira na kuruhusu kila mtu apeleke mpira tena mpaka kurudi kwa mtu wa kwanza. Sasa unaweza kutumia mpira tena.

**Tafakuri**
Waulize washiriki wanalionaje zoezi hili. Wanaitazamaje dhana ya 'mtandao'? Zoezi hili bila matatizo yoyote litakwenda katika zoezi linalofuata 4.2 'Majadiliano ya kimya ukutani'. Katika zoezi hili vijana watatengeneza maana ya 'mtandao'.

***Dondoo***

Endapo huna mpira wa sufi, unaweza kujitengenezea mmoja. Tengeneza mpira kutoka kwenye karatasi na mkanda, zungushia kamba kote kiasi cha kutosha kwa mtandao wa kikundi chako. Unaweza kutumia mstari wa kuosha au kamba yoyote. Unaweza kuwaacha washiriki kutupa mpira bila utaratibu kwa kila mmoja, lakini pia waombe washiriki kutupa mpira kwa mtu ambaye:
- anaishi karibu;
- ni mkubwa zaidi;
- ni mkubwa kidogo kiumri;
- anafanya mazoezi ya michezo sawa;
- ana kazi nzuri.

# 4.2 MAJADILIANO YA KIMYA UKUTANI

**Lengo**
Vijana waunde maana ya dhana ya ‘uundaji mtandao’.

**Maandalizi**
Weka meza kwa namna ambayo vijana wanaweza kufanya kazi katika makundi ya watu watatu. Pia andaa zoezi hili kwa ajili yako mwenyewe kama mkufunzi, ili uweze kujibu maswali yao kwa njia sahihi. Hakikisha kuna karatasi za kutundika za kutosha (chati mgeuzo), gundi ya karatasi, na kalamu za wino mzito kadhaa.

**Maelezo**
'Siku hizi inaonekana kama mitandao imekuwa njia ya kisasa ya kufikia malengo yako kama mtaalamu. Kuna aina zote za makundi ya mitandao. Pia kuna malipo ya kazi, ambapo vijana na wanaotafuta kazi wanaweza kukutana na waajiri na wajasiriamali. Katika mikutano hii vijana watayajua makampuni na hii inaitwa 'mitandao'. Watu wengi wanafikiri kuwa mitandao ni juu ya kutoa kadi yako ya biashara kwa watu usiowajua. Lakini hiyo si sawa kabisa. Ni zaidi kuhusu kujua uhusiano wako na kujaribu kupata msaada kutoka kwao unaohitaji kuongeza fursa zako za kazi. Kila mtu ana mtandao na hata bila kadi ya biashara unaweza kufikia mtandao wako. Katika zoezi hili, tutafuatilia pamoja maana za ‘mitandao’ katika mtazamo wako.’

**Utendaji**
1 Kwanza, ruhusu kila mshirki kujibu maswali yafuatayo:
   - Ni mashirika/vikundi vipi wewe ni mwanachama? Hili linaweza kuwa kundi/shirika ‘Hai’ (kilabu ya mazoezi, kundi la marafiki) au taasisi/kundi la kweli (kundi la mawasiliano, Facebook au kundi la kwenye mtandao wa whatsapp).
   - Je, mashirika/vikundi hivi vina wanachama wangapi?

2 Waagize washiriki waandike ubaoni/kwenye karatasi maneno ambayo, kwa mujibu wao, yanahusiana na dhana ya ‘mtandao’ kila baada ya mshiriki mmoja kuandika neno ampatie mshiriki mwingine kalamu. ‘Majadiliano haya ya kimya ya ukutani’ husimama baada ya chemsha bongo kuisha na wakati hakuna mtu mwingine anaefikiria neno jipya.

3 Tafakari na wanakikundi wenzako juu ya maneno yaliyoandikwa ubaoni/kwenye karatasi. Je, inawezekana kuingiza maneno katika makundi au mada fulani? Mada zipi zinaweza kutofautishwa? Na ni maneno gani yanaingia katika mada hiyo? Andika mada nyingine kwenye karatasi ambazo zinaingia kwenye mada mahsusi, rangi, namba au herufi hiyo hiyo.

4 Gawanya kundi katika makundi ya watu watatu na acha kila kundi litengeneza fasiri (maana) ya dhana ‘mtandao’. Kwa kutumia mada na maneno ambayo yalitokana na majadiliano ya kimya. Weka ukomo wa muda. Kila kundi la watu watatu litaandika maelezo yao ya dhana ya ‘mtandao’ kwenye katarasi.

5 Jadili maelezo/fasiri tofauti katika kundi zima. Je, kuna mfanano wowote? Piga mstari maneno au vifungu vya maneno (virai) ambavyo vinapatikana kwenye maana/fasiri zaidi ya moja. Je, wanaona utofauti (mkubwa)? Ni vipi vipengele muhimu vya dhana ya ‘mtandao’.

6 Mwisho, kundi zima liamue ni maelezo gani yanatakiwa yaingizwe kwenye fasiri/maana ya mwisho. Andika maana ya mwisho kwenye moja ya karatasi. Waelekeze washiriki kuiandika maana hiyo kwenye madaftari yao.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanavyofikiri kuhusu namna walivyofasiri dhana ya ‘mtandao’. Je, ni tofauti na kukariri fasiri/maana kutoka kitabuni. Tofauti ni nini? Njia gani ya kujifunza inafaa zaidi? Na kwanini?

***Dondoo***
Himiza vijana kuandika maneno mengi kadri iwezekanavyo na wazuie wasijadiliane juu ya kile kilichoandikwa wakati wa ‘majadiliano ya kimya kwenye ukuta’. Cha msingi ni ujazo, sio ubora kwa njia hii ya chemsha bongo. Unaweza kuharakisha zoezi hili la chemsha bongo kwa kutumia kalamu mbili za wino mzito na karatasi mbili. Kisha unaweza kuwapa washiriki wawili fursa ya kuandika kile wanachofikiria wakati huo huo. Usitoe maoni yoyote wala kusahihisha kitu chochote, hata kama maneno mengine yametumiwa mara mbili.

# 4.3 JE, MTANDAO WANGU UNAONEKANAJE?

**Lengo**
Vijana watoe taswira ya mtandao wao na wajue mtandao wao unavyoweza kuwa mkubwa.

**Maandalizi**
Fanya zoezi mwenyewe; taswira yako mwenyewe inaweza kutumika kama mfano. Zaidi ya hayo, hii inakupa wewe nafasi ya kujibu maswali yote katika njia inayofaa zaidi. Panga chumba katika hali ambayo vijana wanaweza kuzibandika karatasi zao ukutani na kila mmoja anaweza kutembea kuzunguka ili apate kuona. Hakikisha una karatasi kubwa, kalamu ya wino mzito, na gundi ya karatasi.

**Maelezo**
'Kitu bora kuhusu mtandao ni kuwa kila mmoja anao. Haijalishi ni mkubwa au mdogo kiasi gani au ni jinsi gani unafahamiana na watu. Au namna unavyowajua watu vizuri. Unaweza kutumia mtandao wako kwa njia nyingi. Ili kuonesha ni jinsi gani mtandao ni mkubwa utauangalia kwa kuchora ramani kichwani.'

**Utendaji**
1. Acha washiriki waandike majina yao katikati ya karatasi.
2. Kisha, waandike aina ya watu wote kuyazunguka majina yao wanaoweza kuwafikiria kama vile: familia, vyama vya kitaaluma/vikundi, kazi, marafiki, dini, michezo, majirani, na kadhalika.
3. Kwa kila kundi moja, wanatakiwa kuja na angalau majina 3 ya watu wanaingia kwenye kundi hilo.
4. Waache waning'inize karatasi zao ukutani, ili waweze kuangalia na kuuzungumzia mtandao wa kila mmoja.
5. Waulize kama wanataka kumuongeza mtu yeyote kwenye mtandao wao, baada ya kuona mtandao wa kila mmoja.
6. Ruhusu washiriki kupiga picha ya mtandao wao, ili kwamba wakati wote waweze kuuangalia.

**Tafakuri**
Waulize vijana jinsi wanavyojisikia kuhusu picha walizowasilisha kwenye mtandao wao. Nini kinatokea? Je, kuna tofauti kati ya mitandao mbalimbali katika kundi? Je, wanafikiri wanaweza kutumia mtandao wa washirika wao? Kamilisha zoezi hili kwa kuwaambia vijana jinsi gani utaendelea na mada hii katika masomo yafuatayo: jinsi ya kujenga, kutumia na kudumisha mtandao.

***Dondoo***

Hakikisha vijana wanashirikiana vizuri wanapoangalia mtandao wa kila mmoja. Inachukua muda mwingi na inachosha sana kumruhusu kila mmoja kuwasilisha mitandao yao kwa kundi zima. Unda vikundi vidogo vilivyochangamana kupitia karatasi hizo kama mshiriki bado yupo ili kutoa ufafanuzi mfupi. Inaweza kuleta vurugu kidogo, lakini hiyo ni nzuri ilimradi kila mtu amewasilisha mtandao wake kwa angalau kundi moja. Unaweza pia kuleta muundo zaidi kwa kuunda kikundi cha watu wanne ambao watawasilisha na kujadili mitandao yao kwa awamu.

# 4.4

# PICHA YA MTANDAO WANGU

KARATASI YA ZOEZI 4.4

**Lengo**
Vijana watengeneze mchoro wa mtandao wao na wajue mtandao wao wajifunze kuufafanua.

**Maandalizi**
Waelekeze washiriki wiki moja kabla ya kipindi hiki kuleta simu zao za mkononi. Anuani ya barua pepe inaweza kufaa kutengenezea mtazamo wa jumla wa mtandao wa mtu. Chora kwanza mtandao wako mwenyewe. Chunguza namna mtandao wako ulivyotengenezwa na angalia kama maelekezo katika karatasi ya kufanyia kazi yametoa taarifa ya kutosha namna mtu mwingine anavyoweza kuuchora mtandao wake. Andaa chumba katika hali ambayo washiriki wanaweza kufanya kazi katika jozi. Hakikisha kuna vitendea kazi vya kutosha, karatasi za muundo wa A3, penseli, kalamu za wino mzito zenye rangi tofauti. Chapisha karatasi ya zoezi 4.4.1 'Kuuchora mtandao wangu' na karatasi ya zoezi 4.4.2 'Kuuchanganua mtandao wangu'.

**Maelezo**
'Sote tuna mitandao ingawa mara nyingi tunaweza tukawa hatulijui hilo. Kila mmoja amamjua mtu fulani na mtu huyo ni sehemu ya mtandao wako. Ni rahisi hivyo, kuwa na mtandao mzuri ni mtaji wako wa kimahusiano. Hili ni muhimu sana siku hizi kwa sababu unaweza kuwatumia watu katika mtandao wako kama mtaji. Kwa mfano, mtu fulani katika mtandao wako anaweza kuwa anajua kampuni ipi inayohitaji wafanyakazi. Au mtu fulani katika mtandao wako anaweza kukuambia wewe wapi pa kwenda kwa ajili ya mafunzo ya utendaji. Unaweza pia kumuuliza mtu kutoka katika mtandao wako akueleze zaidi kuhusu kazi zao. Kwa njia hii, unaweza kugundua iwapo hii aina ya kazi inaweza kukufaa. Kuwa na mtandao mkubwa inasaidia sana na ni muhimu. Katika zoezi hili, unaenda kuunda ramani ya mtandao wako kwa kuchora mchoro.'

**Utendaji**
1 Acha kila mshirikia aandike makundi yote ya watu wanaowajua kwenye karatasi tofauti. Mfano wa makundi ni kama: familia, mwenza, mwanadarasa, rafiki, majirani n.k.
2 Watapomalizana na hili, wanaweza kuanza kuchora mtandao wao. Tazama maelekezo kwenye karatasi ya zoezi 4.4.1 'Kuchora mtandao wangu'.
3 Ruhusu washiriki kuangalia kwa umakini kwenye michoro yao kabla ya kuionesha kwa wengine: 'Fikiri tena iwapo watu katika mtandao wako kama wanafahamiana. Utakapoona ni muhimu bado unaweza kuongeza watu wapya kwenye mchoro wako'. Baada ya hili, acha washiriki wawape kila kundi rangi na waruhusu wajibu swali la 11 – 16 kwenye karatasi ya zoezi 4.4.1:
   - Kuna makundi mangapi kwenye mchoro wa mtandao wako (kuna rangi tofauti ngapi)?
   - Ni zipi sifa za makundi haya?
   - Kundi lipi lina watu wengi zaidi?
   - Kundi lipi lina mistari mingi inayounganika zaidi na makundi mengine?
   - Kundi lipi lina mistari michache zaidi inayoungika na makundi mengine?
   - Je, kuna watu wanahusiana na wewe na wewe huhusiani na moja ya makundi yako?
4 Waache washiriki waning'inize michoro yao ukutani na waruhusu wapige picha kupitia simu zao.
5 Kisha acha wachiriki wachambue michoro-mitandao yao kwenye makundi ya watu wawili wawili. Katika hili, tumia maswali kwenye karatasi ya zoezi namba 4.4.2 'Kuuchanganua mtandao wangu'. Majibu ni chachu ya tafakuri kwa kundi zima.

**Tafakuri**
Waulize vijana kuhusu namna wanavyouona mtandao wao. Waaalike washiriki kuwaeleza nini wamegundua katika kuueleza mtandao na wanakundi wenzao. Kundi lipi limetoa msaada mzuri kwao kwa wakati huo? Waeleze ni kwanini?

***Dondoo***
Tembea kuangalia kundi lako na kutoa msaada kwa mtu mmoja mmoja na pale wanapokuwa na maswali au wakati hawakuelewa maelekezo kutoka kwenye karatasi.

# 4.5

# UHUSIANO WANGU NA WATU NINAOWAFAHAMU UNA NGUVU KIASI GANI?

KARATASI YA ZOEZI 4.5

**Lengo**
Vijana wafikirie vile mtandao wao unavyoonekana: watu wanaowajua, wanachokifanya, kwa kiasi gani wanawafahamu, na jinsi wanavyohusiana.

**Maandalizi**
Tafuta jinsi uhusino wako ulivyo na nguvu na watu katika mtandao wako mwenyewe. Unawajua kiasi gani? Unajua nini kuhusu kazi walizonazo? Ni maswali yapi unaweza kuwauliza wao? Kwa kufanya zoezi hili mwenyewe wewe uandae mifano kwa vijana. Zaidi ya hayo, uwe tayari kujiandaa kuyatoa haya mafunzo katika kundi lako. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 4.5.1 'Mtandao wangu kazi na nguvu ya mahusiano' na karatasi ya zoezi 4.5.2 'Duara la mtandao wangu' kama haiwezekani kuchapisha, unaweza pia kuchora azimio kwenye ubao au karatasi. Kama ndivyo, hakikisha kuwa kuna penseli za rangi kwa ajili ya washiriki kuchora duara za rangi katika madaftari yao.

**Maelezo**
'Tambua kwamba mara nyingi hatuzijui kazi walizonazo watu wa kwenye mitandao yetu. Kama una fikira huru: unapata kujua zaidi kuhusu watu unaokutana nao. Na unapojua zaidi, unapata mawazo kuhusu maswali unayoweza ukawauliza. Mahusiano yote ni tofauti. Tunawajua baadhi ya watu kuliko wengine. Kuuliza maswali kuhusu kazi yako ya baadaye. Ni vizuri kuwasiliana na watu unaowachukulia kuwa 'marafiki wazuri' na wale ambao mna mawasiliano ya mbali. Katika zoezi hili, tunaenda kutafuta nani mwenye mahusiano yenye nguvu (urafiki mzuri) na nani mwenye mahusiano dhaifu (mawasiliano ya mbali/marafiki).'

**Utendaji**
1. Washiriki (katika jozi) wanong'one au kuongea kuhusu ni wapi wana nguvu na wapi ni dhaifu katika kuwasiliana nao kwenye mitandao yao?
2. Kuwa na mjadala mfupi katika kundi zima kuhusu tofauti kati ya sifa hizi mbili. Baadaye, wape karatasi ya zoezi namba 4.5.1 'Mtandao wangu' kazi na nguvu ya mahusiano'.
3. Waache washiriki wajaze safu tatu za mwanzo wao wenyewe: watu wanaowajua, kivipi wanawajua na kazi walizonazo. Bada ya hili, wajaze nguvu ya mahusiano yao: ni jinsi gani wanawafahamu vizuri hawa watu?
4. Wape karatasi ya zoezi 4.5.2 'Duara la mtandao wangu' na waelekeze vijana wawaweke hao watu wanaowafahamu vizuri kwenye mduara wa kijani, waweke hao watu wanowafahamu kiasi kwenye duara jekundu na wanaowafahamu kidogo kwenye duara la bluu.
5. Vijana waendelee na hatua ya 2 (kuchora mistari kati ya watu wanaofahamiana) na hatua ya 3 (pima mtandao wako) kwenye karatasi ya zoezi 4.5.2.
6. Washiriki wajadiliane na kupima karatasi zao katika makundi yao yale yale ya watu wawili kama kwenye mwanzo wa zoezi.

**Tafakuri**
Jozi zitakapokuwa zimebadilishana vya kutosha, wakaribishe kujadiliana walichokigundua kwenye kundi zima. Wamegundua nini wakati wakifanya kazi kwenye karatasi ya maswali? Ilikuwaje kwao kuujua mtandao wao na kuyaweka majina katika miduara? Labda mmoja wa washiriki anaweza kueleza ni msaada gani kwa maendeleo ya taaluma yake atahitaji kuwa nao kutoka katika mtandao wa mawasiliano yake? Atakuwa ni rafiki mzuri au mmoja kati ya watu ambao mna mawasiliano ya mbali? Na kwanini?

***Dondoo***

Watie moyo washiriki kuuangalia kwa makini mtandao wao. Kipi kinawashangaza? Waelekeze wahojiane katika makundi ya watu wawili. Tembelea kuzunguka darasa, simama katika kundi lolote na sikiliza ni yapi wamepata; Ikibidi, uliza swali la ziada au la kiundani. Mifano ni: Nani katika mitandao yao watamuomba msaada? Nani wanaweza wakamuuliza swali lipi? Na kwanini? Ni kwanini 'watu ambao mna mawasiliano ya mbali' wanaweza kutumika kukuza fani/taaluma zao? Na ni vipi 'rafiki mzuri' anaweza kuwa wa msaada?

# 4.6

# KUFAFANA NA KUTOFAUTIANA KWA MTANDAO WANGU

KARATASI YA ZOEZI 4.6

**Lengo**
Vijana wachunguze kufanana na kutofautiana kati ya washirika wa mtandao wao. Kwa vipi mtandao wao unatofautiana.

**Maandalizi**
Pia katika jambo hili, ni vyema ukilifanya hili zoezi wewe mwenyewe. Kwa njia hii unaweza ukaona ni jinsi gani mtandao wako umesambaa na jinsi mtandao wako kijamii unavyoonekana. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 4.6 'Mfanano na utofauti katika mtandao wangu'. Badala ya karatasi unaweza ukaandika kwenye ubao kabla ya kipindi kuanza na katika hili vijana wanatakiwa kutumia madaftari yao.

**Maelezo**
'Tangu ulipozaliwa, umekuwa ni sehemu ya kundi fulani. Una wazazi majirani, kaka/dada, n. k. Hawa wanaokuzunguka, tunauita 'mtandao wako wa kijamii'. Huu mtandao unakua kiasili kila wakati unapokutana na watu wapya ambao unaendela kuwasiliana nao kila siku. 'Kutengeneza mtandao' ni kitu cha asili ambacho kila mmoja anafanya. Inaanza na utashi na kuvutiwa na watu wengine. Ni jambo la kutoa na kushirikiana. Mnafahamiana na hii ni sababu kwanini una utayari wa kusaidia wengine na waombe wengine kukupa msaada pindi utakapouhitaji. Ukweli ni kwamba watu unaowafahamu wapo kwa ajili yako, unaufanya mtandao wako kuwa wa thamani kubwa. Kwanini? Kwa sababu watu wanaokuzunguka wanaathari kubwa kwenye kile unachokipata katika maisha na kwa njia gani. Wana athari pia kwa vile utakavyokuwa baadaye. Kufahamu unaowafahamu ni muhimu kama ilivyo muhimu kufahamu vipawa vyako ni vipi kile unachokitaka kukipata katika maisha yako. Kuwajua watu na kuwa na watu wanokufahamu, kuwa na mtandao sahihi, hivyo ni muhimu kutimiza malengo yako katika maisha. Wewe ni yule unayejifahamu. Katika zoezi hili, tunaenda kubainisha ni tofauti na mfanano upi uliopo kati yako na watu wa kwenye mtandao wako. Kwa kufanya hivi, unaweza kugundua mfanano na utofauti uliopo kwenye mtandao wako. Kwa njia hii, unaweza kuona kama kuna watu wa kutosha kwenye mtandao wako unaoweza kuwauliza maswali kuhusu elimu yako, utaalamu na kazi.'

**Utendaji**
1. Tambulisha dhima ya zoezi hili na badilishana mawazo na kundi lako kuhusu 'Kwanini ni muhimu kuchunguza mfanano na utofauti kati ya watu kwenye mtandao wako'.
2. Wape karatasi ya zoezi 4.6 'Mfanano na utofauti katika mtandao wangu' na toa maelekezo kuhusu namna washiriki watakavyoijaza orodha.
3. Baada ya kujaza orodha, waiangalie wakiwa katika makundi ya watu wawili na kujibu maswali yafuatayo:
   - Upi ni mfanano na utofauti kati ya watu kwenye mtandao wangu?
   - Ninaweza kwenda na aina ipi ya maswali kuhusu ukuzaji wa fani yangu kwa watu hawa?
4. Ruhusu kila kijana mmoja mmoja kufanya hitimisho kama wanafikiri mtandao wao unatofautiana vya kutosha kuuliza maswali yao kuhusu maendeleo ya kazi zao.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanaotaka kushirikisha hitimisho lao kwa kundi zima. Uliza ni kwa sababu gani. Kwanini wanafikiri mitandao yao inatofautiana vya kutosha au hapana? Washiriki wengine wanafikiria vipi kuhusu hili? Mtandao uliosambaa una faida gani? Je, wanaweza kufikiri juu ya utendaji au shughuli ambazo zitapanua mtandao wao? Hii inaweza kujadiliwa sana katika kusanyiko lijalo.

***Dondoo***

Tumia matini katika sehemu za maelezo kutambulisha somo kwa namna shirikishi. Katika namna za kuuliza na kujibu au kunong'ona katika jozi, washiriki wataelewa dhamira vizuri kuliko unapowaeleza mawazo yote kwa njia ya maelezo katika sehemu hii.
Wakati watu katika jozi wanazungumza, ni vizuri kutembea katika chumba na kusikiliza hapa na pale nini makundi yanazungumzia. Inapolazimu unaweza ukawasaidia, au kuuliza swali la nyongeza. Hata hivyo, hakikisha huongozi majadiliano yao. Kwa kutoa maoni kidogo na kusikiliza unaweza kutoa mwelekeo kwenye tafakuri mwishoni mwa zoezi.

# 4.7

# NI FANI ZIPI ZINAJITOKEZA KATIKA MTANDAO WANGU?

KARATASI YA ZOEZI 4.7

**Lengo**
Vijana watengeneze ramani ya mtandao wao kwa kutaja fani kwa watu wanaowafahamu. Wanapata uelewa mzuri kwa namna gani watu tofauti kwenye mtandao wao wanavyoweza kuwa wa manufaa kwao.

**Maandalizi**
Fanya hili zoezi ili kuupata uelewa wa somo zaidi. Panga chumba kwa namna ambayo vijana wanaweza wakafanya kazi katika makundi ya watu wanne wanne. Hakikisha kuna nakala za kutosha za karatasi ya zoezi namba 4.7.1 'Taaluma walizonazo watu katika mtandao wangu' na karatasi 4.7.2 'Watu ninaoweza kuwaomba msaada'. Wakati vijana wanahitaji kutumia madaftari yao wenyewe, waandikie mfano wa ramani ya mtandao kwenye ubao kabla ya darasa kuanza.

**Maelezo**
'Watu unaowajua wanaweza kukusaidia kubaini kitu unachomudu na nini unachokipenda. Wanaweza kukusaidia kuchunguza kipi unadhani ni muhimu na ambapo unavutiwa napo. Na wakati unapotaka kupata uzoefu katika shughuli fulani au sekta fulani maalumu, wanaweza wakakutambulisha katika kampuni au mjasiriamali. Je, unahitaji msaada au ushauri? Hivyo wasiliana na watu unaowafahamu. Unaweza ukawauliza kuhusu kazi zao au mafunzo waliyoyafanya. Pia Unaweza ukawaeleza kuwa unatafuta sehemu ya mafunzo ya mazoezi na omba vidokezo. Ni vizuri kufikiri kabla ya nini cha kumuuliza nani, badala ya kuuliza vitu vyote kwa watu unaokutana nao bila kutarajia. Maandalizi mazuri huanza kwa kufikiri kuhusu nani unayemfahamu na nani unaweza kumuomba msaada. Huenda, kila mmoja unayemfahamu yuko tayari kukusaidia, lakini unahitaji watu maalumu kwa malengo tofauti. Katika zoezi hili, tutaanza kufanya uchunguzi kuhusu shughuli inayopatikana katika mtandao wako.'

**Utendaji**
1 Anza zoezi kwa marudio ya vipindi vilivyopita kuhusu mitandao. Lipi lilikuwa somo na waligundua nini?
2 Husisha kati ya masomo yaliyopita na utangulizi wa dhima ya somo hili: kuuangalia mtandao na kuzihusisha fani za watu katika mtandao.
3 Acha mshiriki mmoja mmoja ajaze karatasi ya zoezi 4.7.1 'Taaluma walizonazo watu katika mtandao wangu'. Watengeneze orodha ya majina 30 na fani wanazohusiana nazo.
4 Katika makundi ya watu wanne, washiriki wabadilishane karatasi za zoezi. Watakapomfahamu mtu fulani katika mtandao wa mwakikundi mwenzao, wanaweza wakamuongeza kwenye karatasi yao. Kwa njia hii, karatasi nne zimebadilishwa na kujazwa taarifa mpya.
5 Ruhusu kila mshiriki achague watu wawili (na fani zao) kutoka kwenye orodha yao. Waeleze katika makundi madogo ni maswali au masomo yapi ni sahihi kuwauliza watu hawa wawili. Washiriki wanatakiwa kujadili ni kwanini wamewachagua watu hawa wawili.
6 Acha vijana watengeneze orodha ya watu wanaotaka kuwauliza maswali kuhusu uendelezaji wa fani zao: angalia karatasi ya zoezi 4.7.2 'Watu ninaoweza kuwaomba msaada'.

**Tafakuri**
Waulize vijana kuhusu uzoefu walioupata katika zoezi hili. Wamegundua nini kuhusu watu na taaluma zao uliopo kwenye mtandao wao? Mtandao wangu unatofautianaje na wao? Nani wanaweza kumpendekeza kwa wengine? Je, huyu ni mtu wa kumkaribisha kwa ajili ya uwasilishaji katika kundi hili? Ni kipi mtu huyu anatakiwa kutoa? Ni, kwanini anavutiwa? Maliza zoezi kwa kuangalia darasa litakalofuata, ambapo hatua inayofuata ya kuutengeneza mtandao utafanyika.

***Dondoo***
Kwa kulifanya zoezi hili inakuwa wazi kwamba unaweza ukaupanua mtandao wako kwa kutumia mahusiano ya wanakikundi wako. Bila shaka, hili linatakiwa kufanywa kwa umakini. Wakati vijana wanafanya kazi katika makundi ya watu wanne, unaweza kusikiliza kile ambacho kundi moja linachozungumiza na kwa hali hiyo toa maoni kwani watakuwa wanatengeza mtandao wao sasa. Kwa kubadilishana mawasiliano, wanasaidiana. Katikati ya zoezi, wape maelekezo ya kujaza karatasi ya zoezi 4.7.2 'Watu ninaoweza kuwaomba msaada'.

# 4.8

# MSAADA WANGU KWA WENGINE

KARATASI YA ZOEZI 4.8

**Lengo**
Vijana watafakari msaada ambao wamewapa wengine mwezi uliopita. Wajenge sifa zao na uzoefu ambao unaweza kutumika kusaidia wengine siku zijazo.

**Maandalizi**
Andaa kipindi hiki kwa kufanya zoezi wewe mwenyewe. Andaa chumba katika hali ambayo vijana wanaweza kufanya kazi katika makundi ya watu watatu. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 4.8.1 'Msaada wangu kwa wengine' na karatasi ya zoezi 4.8.2 'Watu ninaoweza kuwaomba msaada', au iweke matini ubaoni kabla darasa halijaanza.

**Maelezo**
'Kutengeneza mtandao inahusu kuomba msaada na kutoa msaada. Wakati mwingine unaweza ukafanya kitu kidogo kwa jitihada ndogo, ambayo kwa ukweli inamsaidia mtu. Vile vile, kupokea msaada mara zote huanza kwa kutoa msaada. Hii inatwa 'kanuni ya kutendeana': unapomsaidia mtu kwanza, baada ya muda utapata msaada wake kama malipo. Ni jambo la kupendeza kuwa na uwiano kati ya msaada unaopokelewa kutoka kwa mtu na msaada unoutoa kwa mtu. Katika zoezi hili, utaangalia ni msaada gani unaweza ukautoa kwa watu wengine.'

**Utendaji**
1. Tambulisha dhima kwa kutumia maelezo. Hamasisha washiriki kufikiri kwa kuwaeleza kufafanua dhana 'kuomba msaada na kutoa msaada' na 'kanuni ya kusaidiana'. Kwanza, waache waunde mawazo yao kabla ya kueleza maana ya zoezi.
2. Acha kila mmoja ajibu maswali kwenye karatasi ya zoezi 4.8.1 'Msaada wangu kwa wengine'.
3. Ruhusu kila kijana abadilishane na kujadili majibu yake katika makundi ya watu watatu. Kila mmoja atoe mrejesho kwa mwenzake kuhusu aina ya msaada wanaoweza kutoa:
   - vitu wanavyovifahamu sana kuhusu;
   - vitu wanavyoweza wakavifanya vizuri;
   - kutengeneza mtandao: watu wenye mvuto ambao wanaweza wakawatambulisha kwa wengine.
4. Wape kazi ya nyumbani kuwauliza watu katika mazingira yao ni aina gani ya msaada wanaweza kuitoa.
5. Waelekeze vijana kuandaa orodha ya watu wanaotaka kukutana nao kwa lengo la kuwaomba msaada unaohusu maendeleo ya kazi zao, angalia karatasi ya zoezi 4.8.2 'Watu ninaoweza kuwaomba msaada'.
6. Kubaliana kuhusu namna ambayo kazi ya nyumbani itajadiliwa katika kipindi kitakachofuata na jinsi karatasi ya zoezi 4.8.2 'Watu ninaoweza kuwasaidia' itakavyomaliziwa.

**Tafakuri**
Waulize washiriki wamejifunza nini kutokana na zoezi hili. Wamegundua nini kuhu 'kanuni ya kutendeana'? Vipi kuhusu uhusiano baina ya 'kutoa na kupokea msaada'? Kuna uwiano wowote, na nini kinatokea kama hapana usawa? Vijana wamepata mambo mapya katika sifa zao kwenye zoezi hili? Kama ndiyo, yapi? Nani ana watu anaowasiliana nao wanaovutia anaeweza kuwapatia?

***Dondoo***
Katika utangulizi, vijana waunde mawazo yao binafsi kuhusu dhana ya 'kuomba na kupokea msaada' na 'kanuni ya kutendeana'. Usitoe maana yako mwenyewe mapema na kuhusisha moja kwa moja na uzoefu walionao washiriki kuhusu kuomba na kutoa msaada. Washiriki wanaweza wakawa wananong'ona, kuongea katika makundi kuhusu dhana unayoandika ubaoni. Njia shirikishi inaongeza ushiriki kwenye somo. Hakikisha vijana wanaongeza kwenye karatasi ya zoezi 4.8.2 'Watu ninaoweza kuwaomba msaada' wakati wanapofanya kazi katika makundi ya watu watatu au kwenye kundi zima.

# 4.9

# NI MSAADA GANI NAWEZA KUUTUMIA?

KARATASI YA ZOEZI 4.9

**Lengo**
Vijana wajifunze kuunda maswali ya wazi na thabiti kwa msaada kuhusu maendeleo yao ya kazi zao.

**Maandalizi**
Kujifunza kuuliza maswali mazuri kunahitaji mazoezi. Swali dhahiri huleta jibu zuri. Inasaidia katika kulifanyia kazi zoezi la kuuliza maswali wewe mwenyewe. Kwa njia hii, unajiandaa vizuri kutoa mrejesho. Andaa vitu vinavyohitajika katika kufanyia mazoezi kwa ajili ya msaada. Hakikisaha unazo nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 4.9 'Ni msaada gani naweza kuutumia?' au andika dondoo za karatasi kwenye ubao.

**Maelezo**
'Hata kama una mtandao mkubwa, uliotawanyika na unaopendeza kama huwaombi watu msaada hawatakusaidia. Kupata msaada unaouhitaji kutoka kwenye mtandao wako, unahitaji kuuliza maswali dhahiri. Unaweza ukajifunza hili kwa kufanya majaribio na mazoezi. Inasaidia unapoongea na watu na kuwauliza maswali kuhusu masomo, kazi na taaluma zao. Hapo utakuwa unawaua ndege wawili kwa jiwe moja, kwa sababu unafanya zoezi la kuwauliza maswali ambayo ni mazuri na unachagua zaidi kile unachokitafuta. Katika mjadala huru, mtu ambaye unaongea naye atafikiria pamoja na wewe. Kama unataka watu wakusaidie, unatakiwa kuunda maswali yanayoendana na mahitaji yako. Hili ndilo tunaenda kulifanyia kazi sasa hivi.'

**Utendaji**
1 Baada ya utangulizi wa dhima 'kujifunza kuuliza maswali mazuri kuhusu maendeleo ya kazi kwa watu katika mtandao wako', waalike vijana kufikiri katika jozi kuhusu kigezo cha swali kuwa zuri.
2 Weka vigezo vyote kwenye karatasi kubwa au kwenye ubao na kuvijadili. Waelekeze vijana kuvieleza vigezo hivyo kwa kutumia mifano midogo. Tengeneza orodha ya pamoja ya vigezo 3-5.
3 Waelekeze washiriki, mmojammoja kufikiri maswali mazuri kuhusu maendeleo ya kazi kwa kuvizingatia vigezo. Kuomba msaada kuanze na: Ninamtafuta mtu ambaye... Angalia karatasi ya zoezi namba 4.9 'Ni msaada gani naweza kuutumia?'
4 Unda jozi na waelekeze washiriki kusaidiana kuboresha mahitaji yao ya msaada na kuunda maswali sahihi kwa watu katika mitandao yao. Angalia karatasi ya zoezi 4.9 'Ni msaada gani naweza kuutumia?'
5 Waelekeze vijana kujaza jedwali kwa majina ya watu ambao wanaweza kuwaomba msaada. Wape kazi ya nyumbani kuwaendea watu wawili au zaidi wa kwenye orodha ile. Waelekeze waandike kwenye karatasi ya majibu ambayo watayapokea.
6 Afiki juu ya tarehe ya kujadili kazi ya nyumbani katika moja ya vipindi vijavyo.

**Tafakuri**
Unaweza kuwaita washiriki kutoa mfano wa swali waliloliboresha katika kundi zima, wakiwa wanaendelea kufanya kazi katika jozi. Kundi lijadili kama hii inasaidia kuvifika vigezo walivyoviunda mwanzoni mwa zoezi. Je, uboreshaji wowote unaweza kuendelea kufanyika. Uliza kundi limejifunza nini kutokana na kufanya kazi kwa namna hii. Angalia vizuri endapo kweli kila mmoja anaenda kuomba msaada kwa watu kwenye mitandao yao, na uwaeleze tena kuhusu tarehe ya kuijadili kazi ya nyumbani.

***Dondoo***
Inashauriwa kwamba washiriki wenyewe wafikiri kuhusu vigezo vya swali halisi. Hii inaongeza uwezo wao wa kufikiri na wanajifunza kumudu masomo na kazi zao. Kwa kulifanya zoezi hili, wanakuwa na wajibu wa kile ambacho wanajifunza. Utafutaji wa maswali yanayofaa zaidi huwafanya vijana kuwa na uwezo wa kujiendeleza wenyewe. Moyo wa kujituma na kuwajibika ni ujuzi muhimu katika karne ya 21 katika kuitengeneza/ kuimarisha kazi.

# 4.10

# MAWASILIANO: UNAWEZA KUJIFUNZA HILI?

KARATASI YA ZOEZI 4.10

**Lengo**
Vijana wajifunze kuhusu umuhimu wa mawasiliano mazuri na yanaweza kuleta athari gani katika mahusiano yao na wengine.

**Maandalizi**
Kama maandalizi, inaweza ikapendeza kuchukua mifano binafsi waliyonayo akilini kuhusu namna yako ya mawasiliano ilivyokuwa na athari chanya. Lakini pia chukua mifano kadhaa kuhusu namna yako ya mawasiliano ilikuwa na athari hasi kwa mtu mwingine, ambapo hili halikuwa lengo lako. Kwa kufanya hivi, unakuwa kama mfano wa kuigwa kwa vijana na unaweza ukawasaidia wanapokuwa na swali lolote. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 4.10 'Maelezo kuhusu namna ninavyowasiliana'.

**Maelezo**
'Katika zoezi hili, tunaenda kuchunguza namna yako ya kuwasiliana inavyowaathiri wengine, mtu mmoja mmoja na kwenye kundi. Namna yako ya kuwasiliana pia inahamasisha kundi lako. Unawasiliana na watu katika hali ambayo wanawiwa kufanya kitu kwa ajili yako? Au unagundua kwamba watu wakati mwingine wanasita unapowaomba kitu fulani? Hii inaweza kuwa inatokana na namna ambavyo unawasiliana. Katika zoezi hili tutaangalia kwa undani kuhusiana na hili. Kwa muda gani umekuwa na uelewa kuhusu namna yako ya kuwasiliana, unaweza ukaibadilisha kama utahitaji kufanya hivyo. Au utakapogundua unaweza ukafanya vitu vizuri, unaweza ukajifunza kuutumia ujuzi huu katika hali mbalimbali.'

**Utendaji**
1 Ligawe kundi lako mara nne.
2 Waombe washiriki kufikiri kimya kimya kuhusu maelezo ya kwenye karatasi ya zoezi 4.10 'Maelezo kuhusu namna ninavowasiliana'. Waelekeze kila mmoja kuweka alama ya vyema kwa kila maelezo. Je, inatokea mara chache, mara nyingi au haitokei.
3 Baadaye, waelekeze kuyajadili baadhi ya maelezo kwenye vikundi vyao. Waache waongeee kwa uhuru. Usitoe maelekezo mengi. Waelekeze washiriki kuhakikisha kila mshiriki katika kundi anasikika na anaweza akamalizia maoni yake. Waelekeze kutoa mrejesho wanapoweza kuona sifa fulani katika maelezo yao.
4 Waelekeze washiriki kufikiri kuhusu zoezi hili linawaeleza nini kuhusu wao wenyewe. Waruhusu wandike na kumalizia sentensi zifuatazo: 'Ninapoangalia mwenendo wa mawasiliano yangu mwenyewe, niko vizuri kwenye...' na 'Ninapoangalia mwenendo wa mawasiliano yangu mwenyewe, nagundua ugumu katika...'.

**Tafakuri**
Waombe washiriki wanne kukuonesha kile walichokiandika kujibu maswali 'Wewe ni mzuri katika kufanya nini?' Waulize washiriki wengine wanne nini walichokiona kigumu katika mawasiliano. Waulize washiriki wengine wanne kama wanajua sehemu zao nzuri na mbaya katika namna zao za mawasilano. Panga miadi na kundi kuhusu lini na namna gani ya kwenda ndani zaidi katika magumu.

***Dondoo***
Tambua kuwa kuangalia namna ya tabia zako za mawasiliano ni vigumu. Ingawa tunawasiliana maisha yetu yote, mara nyingi hatukijui kile tunachokifanya na ni kwa namna gani hili linawaathiri wengine. Zaidi, wote hatuwezi kuona namna ambavyo tunawasiliana. Hivyo, hakikisha vijana wote wanajisikia huru kutafakari hili.

**Uchunguzi wa kina**
Inapokuwa kuna washiriki wengi ambao wanaugumu katika namna fulani za mawasiliano, unaweza ukaandaa mgeni au warsha kwa ajili ya kufundisha mada hii. Unaweza pia ukawaomba wale ambao ni wazuri katika mawasiliano kuwasaidia wanakundi wenzao. Jadili namna wanavyoweza kuwa na msaada.

# 4.11

# SENTENSI ZA MWANZO: UTANGULIZI MZURI NI NUSU YA PAMBANO!

**Lengo**
Vijana wafikiri kuhusu sentensi za mwanzo wanazoweza kuzitumia katika hali ambazo wanapata ugumu kujitambulisha kwa watu wasiowafahamu. Wajifunze kwamba ni muhimu kujiandaa vizuri.

**Maandalizi**
Vipange viti katika mduara bila kuwa na meza. Fikiria baadhi ya mazingira ambapo vijana wanahitaji kweli kuwa na utambulisho mzuri katika ufunguzi wa maongezi.

**Maelezo**
'Wakati mwingine tunaishia katika mazingira ambayo si rahisi. Kwa mfano, kwenda sherehe ambayo humfahamu mtu yeyote. Au kupata kazi ambayo hukuwahi kuifanya. Au siku yako ya kwanza shuleni, kazini au katika mazoezi ya utendaji. Hivyo ni vizuri kufikiri kuhusu utambulisho (sentensi za mwanzo/utangulizi) kabla ya kuchukua hatua. Hii inaweza ikakufanya uwe na hisia kali kidogo, kwa sabau umehakikishiwa kwamba unaweza kuanzisha mazungumzo. Kufanya mawasiliano mazuri kwanza, hasahasa katika hali ambapo kuna watu wengi zaidi, hilo ndilo tutakalolifanyia mazoezi leo.'

**Utendaji**
1. Baada ya utangulizi wa somo, fikiria pamoja kuhusu mazingira ambayo washiriki wanaweza wasijisikie vizuri kwa sababu bado hawamfahamu yeyote. Chagua hali moja kwa hatua inayofuata.
2. Ruhusu kila mmoja aandike sentensi ya mwanzo kwenye karatasi yake kimyakimya.
3. Wazikunje karatasi zao ili washiriki wasiweze kusoma sentensi za ufunguzi za kila mmoja. Kusanya karatasi zote na ziweke kwenye bakuli au kasha.
4. Acha mtu yeyote achugue karatasi, aifungue na kuisoma kwa sauti.
5. Baada ya kila sentensi ya mwanzo, watu watatu wanaweza wakatoa mrejesho kwanini sentensi ni nzuri au mbaya. Rudia hili mpaka karatasi zote zifunguliwe na kusomwa kwa sauti.
6. Mtu mmoja aandike sentensi zote nzuri za mwanzo ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Kila mmoja anaweza kunakili sentensi za mwanzo kwenye madaftari yao.

**Tafakuri**
Liulize kundi linajisikiaje kuhusu kuanza mazungumzo kwa namna hii? Wamezisikia sentensi za mwanzo wanazozifikiria kuwa ni 'hiyo ni sentensi ninayoweza kuitumia katika mazingira ambayo simfahamu yeyote'? Nini wanapenda zaidi?

***Dondoo***
Watie moyo vijana kuwa wa kweli kadri itakavyowezekana; siku zote sentensi zinaweza zikaboreshwa baada ya muda. Kwa kuwafanya vijana waamue haraka kadri iwezekanavyo kama sentensi ni nzuri au mbaya, dumisha kasi ya zoezi. Sentensi za mwanzo ambazo zitazokadiriwa kuwa 'Nzuri' zinawekwa katika makundi na kuandikwa mwishoni. Huenda vicheko vinaweza kutokea, lakini hiyo ni sehemu ya hili zoezi.

**Uchunguzi wa kina**
Kwa kufanya ufuatiliaji, unaweza ukawaelekeza vijana kuandika hali ambazo watakumbana nazo wiki tatu zijazo ambazo watakuwa na aibu kusema baadhi ya vitu. Hizo ni hali ambazo hawatajisikia vizuri. Weka miadi ni lini mtajadiliana hali hizi katika kundi hivyo wanaweza wakatoa mrejesho na kupendekeza.

# NI NANI ANANIVUTIA?

**Lengo**
Vijana wachunguze ni watu gani wanawavutiwa nao au wanawapenda. Lengo la kushirikiana pia ni kusikiliza kwa umakini na kutengeneza muhtasari fasaha.

**Maandalizi**
Ili kujiandaa mwenyewe, itafaa zaidi kulifanya zoezi hili wewe mwenyewe. Fikiria pia kuhusu kigezo cha usikilizaji na ufupishaji mzuri. Kisha unaweza ukajibu vizuri maswali yanayofuata.

**Maelezo**
'Wakati mwingine unaweza ukakutana na watu wanakupendeza kwa sababu wanaweza wakasema vitu fulani kwa namna nzuri. Au kwa mfano, kwa sababu wanaweza kueleza vitu fulani vizuri. Kwa mfano, kuna watu walio wahi kukutana na Nelson au Winnie Mandela walipendezwa sana na namna alivyokuwa akiongea. Katika zoezi hili, tunaenda kuchunguza watu gani unaona wanakuvutia au watu wanaofanya vitu vya kukupendeza. Baada ya hayo, tunaenda kufanya mazoezi ya kusikiliza kwa makini na kufupisha pia.'

**Utendaji**
1. Vijana wawaandike watu wawili ambao wanaowavutia. Hawa wanaweza wakawa watu maarufu (walio hai au wasio hai), inaweza kuwa watu wa kufikirika pia (kwa mfano kitabu au filamu). Lakini pia wanaweza kuwachagua watu ambao sio maarufu sana (familia, marafiki).
2. Baada ya kuandika majina, waombe waandike maneno matatu yanayowaelezea watu ambao wanawavutiwa au kupendezwa nao.
3. Ligawe kundi katika makundi ya watu watatu.
4. Washiriki wajigawe katika makundi ya watu A, B na C.
5. Mtu A sasa aeleze kuhusu watu aliowaandika.
6. Mtu B awe wa kumhoji mtu A kuhusu kile anachopenda kujifunza kutoka kwa watu hao na kwanini. Mtu B aulize zaidi mpaka mtu A aeleze kila kitu anachotaka kueleza kuhusu mtu anayempenda au kuvutiwa naye.
7. Itakapokuwa mahojiano yamekwisha mtu C ajiweke katika nafasi ya mtu A, kwa ufupi ni kusema: 'jina la mtu A anafikiri ..... (majina ya mtu A aliyosema kuhusu) yanavutia, kwa sababu......angependa kujifunza kutoka kwao (uzuri wa mtu A alioueleza).
8. Mtu C amuulize mtu A kama ufupisho huo ni sahihi. Mtu A atoe mrejesho.
9. Mtu B afuate kusema anayemfikiria kuwa anamvutia. Mtu C amfanyie mahojiano na mtu A ayafupishe. Baada ya huu ufupisho wa pili majukumu yabadilishwe tena na mtu C aseme kuhusu watu anaowapenda, mtu A amfanyie mahojiano na mtu B afupishe.
10. Katika makundi ya watu watatu, washiriki wajadili mambo ambayo wamejifunza katika zoezi hili. Wajadili yale waliyojifunza kwa sababu zilizotolewa na watu kuhusu ni kwanini wanavutiwa na watu fulani na wajadili kama wamesikiliza kwa makini na kufupisha vizuri.

**Tafakuri**
Liulize kundi kuhusu jinsi lilivyojisikia kuhusiana na zoezi hili. Je, wamegundua kitu kipya? Walifanyaje katika kufanyia mazoezi ujuzi wa kusikiliza na kufupisha? Je wana maelekezo yoyote ya kujipa wenyewe au kwa wanakikundi?

***Dondoo***
Zoezi hili kimsingi linamaanisha kuwafanya vijana wajue ni nini hasa kinawavutia na nini wanachopenda kwa wengine. Katika zoezi hili, wamegundua vitu wanavyohitaji kujifunza zaidi.

# 4.13

# EHHHH, NI MIMI EHHHH....

KARATASI YA ZOEZI 4.13

**Lengo**
Vijana wachunguze namna ya kuwa na mawasiliano na mtu ambaye hawamjui na namna ya kuanza mazungumzo. Wataibua 'ya kufanya' na 'ya kutofanya'.

**Maandalizi**
Kiandae chumba katika hali ambayo ni rahisi kufanya igizo katika makundi ya watu watatu. Igizo ni njia nzuri kuhamasisha kuziangalia tabia na kuamua kama kuna haja ya kufanya uboreshaji. Kama kuna ugumu wa kufanya igizo, inasaidia kujua ni kwanini kulitumia na kipi kinatakiwa kwa utendaji mzuri. Fanya mazoezi na wenzako kupata uzefu na omba maelekezo kwa ajili ya ushauri wenye mafanikio. Hakikisha unazo karatasi ya zoezi 4.13 'Kuchunguza mahusiano na mazungumzo kwa mara ya kwanza' au andika maswali kuangalia kwenye ubao au karatasi kubwa.

**Maelezo**
'Fikiri kama uko kwenye sherehe ambapo humfahamu yeyote. Au fikiri umeenda kufanya mazoezi kwa utendaji sehemu fulani kwa mara ya kwanza na humfahamu yeyote sehemu hiyo. Au upo kazini sehemu fulani ambapo kuna kazi na makampuni mengi yapo na humfahamu yeyote pale. Utafanya nini? Utamwendea mtu yeyote na kuanza mazungumzo? Na vipi utalifanya hili? Katika zoezi hili, tunaenda kuona ni namna gani tunaweza tukawa karibu na watu ambao hatuwafahamu na kuanza nao mazungumzo. Lipi ni linapaswa kufanywa na lipi halipaswi?'

**Utendaji**
1 Tambulisha dhima na uwakaribishe washiriki kulifanya zoezi mbele ya darasa.
2 Fafanua ukiwa pamoja na washiriki wawili, ni katika hatua gani zoezi linafanyika? Uko wapi? Ni mazingira gani? Ni watu gani unajaribu kuwa karibu nao?
3 Washiriki wengine katika kundi wape wajibu wa kuwa watazamaji. Waandike dondoo kuhusu zipi zilikuwa hoja nzuri katika kuwasiliana na kuanzisha mazungumzo. Maelekezo kwa ajili ya maboresho yanaweza yakachukuliwa. Wanaweza wakaandika mawazo yao kwenye karatasi ya zoezi 4.13 'Kuchunguza mawasiliano na mazungumzo kwa mara ya kwanza' au kwenye madaftari yao.
4 Ruhusu washiriki wawili wafanye zoezi.
5 Baada ya zoezi, kwanza waombe wao kutoa maoni kwa ufupi jinsi zoezi lilivyokwenda. Waelekeze watulie kidogo kwa sasa, kama inavyoweza ya kuogopesha na yenye mawazo katika kufanya zoezi mbele ya kundi zima.
6 Baada ya hili, waulize watazamaji kuhusu kile walichokiona na kipi kilienda vizuri kwa mujibu wao. Je, kuna mapendekezo yoyote ya uboreshaji? Ongeza mrejesho chanya kama utahitajika.
7 Mwisho, uliza mrejesho wa majibu walioupata jozi iliyofanya zoezi. Washukuru kwa mchango wao na waoneshe kukubaliana kwa kuwa na moyo wa ujasiri kufanya zoezi mbele ya kundi zina.
8 Karibisha jozi nyingine kulifanya zoezi hili mbele ya kundi zima pia. Irudie hatua ya 2-7.
9 Baada ya hili, mpe kila mmoja nafasi ya kufanya zoezi. Hii ifanyike katika makundi ya watu watatu. Fuata hatua ya 2-7. Mshiriki mmoja kati ya watatu awe mtazamaji na atumie karatasi ya zoezi 4.13 'Kuchunguza mahusiano na mazungumzo kwa mara ya kwanza' ili kutoa mrejesho. Itakapokuwa tayari, washiriki watatu wajadili mrejesho na kubadilisha nafasi zao ili mshiriki anayefuata apate fursa ya kufanyia zoezi. Hakikisha kila mmoja amehusika katika nafasi tatu tofauti: mmoja anayefanya mawasiliano, mmoja anayefuatwa kuwasiliana na mwingine ambaye ni mtazamaji.
10 Ziweke pamoja hoja 'ya kufanya' na 'ya kutofanya' katika orodha kwenye kipindi cha kuuliza na kutafakari. Waelekeze vijana kutengeneza nakala ya orodha kwenye karatasi zao au madaftari.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanavyojisikia kuhusu njia hii ya kujifunza. Kipi kilikuwa kigumu? Wamegundua nini kuhusu njia zao za kuwasiliana na watu? Hii ina maana gani kwa kujitambulisha katika siku zijazo? Kuna yeyote anaweza kutoa mfano jinsi atakavyokuwa akifanya tofauti baadhi ya vitu katika kipindi kijacho? Andaa orodha 'ya kufanya' na 'ya kutofanya' washiriki watakapokuwa wanaeleza kuhusu ugunduzi wao na vitu watakavyovifanya hivyo hivyo au katika hali ya tofauti.

***Dondoo***

Hakikisha kuna mazingira chanya na salama kwenye kundi unapokwenda kufanya igizo hili. Unaweza kulijua hili kwa kutambulisha kwamba igizo ni zoezi la kawaida ambalo kwalo vijana wanaweza wakajifunza. Kuandaa 'jukwaa' pamoja ni hatua nzuri kwa vijana kwani wanaweza wakayaandaa mazingira ambamo wanaweza wakalifanya zoezi. Hii inaifanya hali kuwa halisi na ya kusadikika kidogo. Kuivuta pumzi na kuitoa nje, kukaa kimya baada ya zoezi na kutoa mrejesho mzuri ni muhimu. Mara nyingi anza na maliza na mrejesho chanya. Unaweza kuwapa maoni ya uboreshaji. Usitoe maoni mengi kwa ajili ya uboreshaji, kwa sababu hii itawafanya washiriki kufikiri kama walifanya makosa mengi. Vijana wakiuliza, 'ni kipi alikifanya vizuri?' na jibu likawa na mrejesho hasi tu, inabidi ulirekebishe kundi. Kuwa mkali kwa hili: maoni hasi hayaruhusiwi. Waelekeze vijana wajue kwamba mrejesho hasi utakuwa wa kutakiwa na kwa kipindi hiki hesabu mambo yaliyoenda vizuri tu.

# 4.14

# MWANAMTANDAO HALISI

KARATASI YA ZOEZI 4.14

**Lengo**
Vijana wachunguze majukumu ya mwanamtandao bora na kupima kazi zao wenyewe zihusianazo na uundaji wa mtandao.

**Maandalizi**
Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 4.14 'Mwanamtandao halisi....' au andika vitu muhimu ubaoni au kwenye karatasi. Kwa maandalizi ni vizuri kulifanya kwanza zoezi mwenyewe. Hivyo unaweza ukawa mfano wa kuigwa kwa vijana na kuwasaidia inapokuwa vigumu katika kufanya shughuli kadhaa za mtandao.

**Maelezo**
'Watu ambao hawako kama wewe, kwa mfano jamaa zako, wanaweza wakakupa kiurahisi maelekezo ambayo hukuyategemea. Wakati mwingine 'marafiki wa mbali' wanaweza kukusaidia kwa maendeleo ya shughuli yako kuliko marafiki wa karibu. Lakini watu usiowajua vizuri ni watu unaowaomba msaada mara chache. Kuomba msaada watu usiowafahamu vizuri, unatakiwa kuhakikisha wasiwe hawakufahamu kabisa. Hii inahitaji nguvu kubwa kuliko kwa marafiki. Unatakiwa kuuendeleza uhusiano wako na watu ambao sio kama wewe. Leo tunaenda kugundua sifa za mwanamtandao mzuri na kile anachokifanya. Kisha, tutaangalia kwenye mtandao wako na shughuli za mtandao huo zinazokupa uhuru.'

**Utendaji**
1. Baada ya utangulizi wa somo unaweza ukawaelekeza vijana kutaja majina ya watu ambao ni wazuri katika kutengeneza mtandao kuonesha shughuli za watu wanazozifanya. Angalia karatasi ya zoezi 4.14 'Mwanamtandao halisi....'.
2. Waelekeze vijana kujadiliana majibu yao katika jozi.
3. Vijana waoneshe mmoja mmoja kwenye karasi zao kitu ambacho wanaweza wakakifanya kuwa na mawasiliano na watu wanaowafahamu.
4. Baada ya hili wajaze azimio na kuona wanalolifanya, lipi linawapa uhuru na linawapa nini.
5. Wajadiliane utafiti wao katika makundi.

**Tafakuri**
Waulize vijana kuhusu shughuli zipi za mtandao wanazozipenda na zipi ambazo daima hawataki kuzifanya. Kwa sababu gani? Shughuli yao pendwa ya kimtandao itawapatia nini? Je, hii inatosha kuwaomba msaada watu wasiowafahamu?

***Dondoo***
Watie moyo vijana waandike kadri iwezekanavyo shughuli za kimtandao kwenye karatasi zao za zoezi, hata kama hawazifanyi au hawazipendi. Ni vizuri pia kufahamu kile ambacho hawatakifanya na sababu zake ni zipi. Kuwa na mtandao ambao upo tofauti nawe sio jambo zuri katika maisha. Hii inaweza kukupa picha halisi ya kile ambacho kinakufaa.

**Uchunguzi wa kina**
Katika mazoezi ya mada 'Matendo yako na kuomba kazi' zoezi 6.11 'Mpango kazi wa mtandao wangu' umejumuishwa. Kama unataka kuendelea na shughuli zaidi za uendeshaji kwa utekelezaji wa hatua kama mrejesho wa mazoezi kuhusu kuendeleza mtandao, unaweza kupanga ratiba kwa ajili ya darasa linalofuata.

# 4.15

# NA KISHA KUKAWA NA UKIMYA.......

KARATASI YA ZOEZI 4.15

**Lengo**
Vijana wachunguze mazingira ambamo walikwama kwenye mazungumzo. Wanafaya mazoezi ya namna ya kuendeleza mazungumzo kwa lengo la kutengeneza mahusiano ya kimtandao.

**Maandalizi**
Itazame kwa umakini karatasi ya zoezi 4.15 'Hatua katika kuwasiliana'. Je, hatua zinaendana na namna ya kuingiliana ambayo ni ya kawaida katika jamii yako? Kuna tofauti kubwa na ndogo zinazoweza kuwepo kwa kila tamaduni. Ikilazimu, rekebisha maelezo kwenye karatasi au ifanye hiyo pamoja na kundi lako. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi. Jifunze igizo na wenzako ikiwa hulifahamu vizuri zoezi hilo.

**Maelezo**
'Kuwasiliana na mtu usiyemfahamu ni vigumu. Kama huwezi kuyafanya mazungumzo yaendelee, haiwezi kuwa rahisi kukutana na mtu wa hivyo. Labda umeipitia hali ya namna hiyo. Uliwasiliana na mtu fulani, ulianzisha mazungumzo, lakini hayakuendelea vyema. Na mtu mwingine hakusema lolote. Ulifikiri kuhusu mada mpya ili kuyaendeleza mazungumzo lakini mwisho ukakosa mawazo. Na hapo ukakata tamaa. Kwa kweli huu sio uzoefu mzuri! Katika zoezi hili, tunaenda kuchunguza na kufanyia mazoezi namna tunavyoweza kuyafanya mazungumzo ya kadumu, hivyo unaweza ukatengeneza kiunganishi kipya katika mtandao.'

**Utendaji**
1 Waelekeze vijana kufikiri na kutafakari katika makundi ya watu wawili kuhusu mada mbili zifuatazo:
   - Uliwahi kuwa na mazungumzo ambayo hukuwa na mafanikio mazuri? Fikiri kuhusu mfano na uwashirikishe kilichoenda vibaya katika mazungumzo hayo.
   - Kwa pamoja andaa orodha inayotakiwa ili kuwa na mazungumzo mazuri.

2 Yajadili matokeo ya vijana. Waulize kinachozuia mazungumzo kuwa mazuri na nini kinachochea. Yaandike majibu yao katika safu mbili ubaoni au kwenye karatasi, safu moja iwe na kinachozuia mazungumzo kuwa mazuri na safu ya pili iwe na kinacho chochea.

3 Baadaye, wapatie karatasi ya zoezi 4.15 'Hatua katika kuwasiliana'. Ruhusu vijana kusoma na kujadiliana katika makundi yale yale ya watu wawili ni kwa kiasi gani wanaweza kuujua uzoefu wao. Ni sehemu zipi kwenye majadiliano zimerudi kwenye nadharia ya kwenye karatasi ya zoezi?

4 Wakaribishe washiriki wawili kufanya mazoezi ya namna ya kudumisha mazungumzo ya awali.

5 Fafanua ukiwa na washiriki wawili ni katika mazingira gani mawasiliano ya mwanzo huchukua nafasi. Uliza maswali kama vile: Uko wapi, ni mazingira yapi na nani anafanya mawasiliano? Andaa 'jukwaa' kulifanya tukio kuwa halisi zaidi.

6 Washiriki wengine waambie wawe watazamaji. Karatasi ya zoezi inaonesha namna ya kutazama. Waelekeze waandike kile kilichoenda vyema katika mazungumzo: Je, yalikuwepo mawasiliano mazuri na je, mazungumzo yalikwenda sawasawa? Dondoo za uboreshaji pia zinaweza kuandikwa.

7 Waelekeze washiriki wawili kulifanya zoezi.

8 Baada ya hapo, kwanza iulize jozi wanavyofikiri waliyofanya. Waambie kwanza waivute pumzi nje, kwa sababu inaogopesha hofu kulifanya hili zoezi mbele ya watu.

9 Baada ya hili waulize watazamaji walichokiona na kipi kilifanyika vyema kwa mujibu wao. Kuna maoni yoyote kwa ajili ya maboresho? Ongeza mrejesho chanya kama utahitajika.

10 Hatimaye, waelekeze washiriki wawili waliolifanya zoezi kutoa mtazamo wao juu ya mrejesho waliopewa na uwashukuru kwa michango yao na uoneshe shukrani kwa kuwa tayari kulifanya zoezi mbele ya kundi zima.

11 Baada ya hili, mpe kila mmoja nafasi ya kufanyia mazoezi 'Kuanza mawasiliano na mtu na kuyaendeleza mazungumzo'. Hii inafanyika katika makundi ya watu watatu. Mmoja kati ya watu watatu ni mtazamaji na anatumia karatasi ya zoezi 4.15 'Hatua za kufanya mawasiliano' ili kutoa mrejesho wake. Baada ya kila zoezi, makundi ya watu watatu yajadili mrejesho na wabadilishane nafasi za uhusika ili mshiriki anayefuata awe na nafasi ya kufanya zoezi. Hakikisha kila mmoja amechukua uhusika wa namna tofauti tatu: kufanya mawasiliano, kufuatwa kwa ajili ya mawasiliano na kuangalia.

12 Karatasi yenye matazamio inaweza ikatolewa kwa washiriki waliokuwa wakifanya mazoezi. Anaweza akatoa maoni kwa mdomo au akaongeza hitimisho lake kwenye karatasi ya zoezi.

13 Jadiliana wakati wa kuhitimisha endapo karatasi ya zoezi 4.15 'Hatua katika kuwasiliana' zinaweza zikaboreshwa pamoja na vidokezo na mitego inayojitokeza wakati wa mazoezi.

**Tafakuri**
Waulize vijana kama wamegundua kitu chochote wakati wa zoezi ambacho hawakujua. Je, ni vidokezo gani wanavyochukua kwenda navyo nyumbani? Tuseme kwamba karatasi ya zoezi 4.15 'Hatua katika kuwasiliana' inaweza kuboreshwa, ni nini kinachopaswa kubadilishwa au kuongezwa?

***Dondoo***

Hakikisha kuna mazingira salama na chanya katika kikundi wakati unapoenda kufanya igizo hili. Unaweza kubaini hili kwa kulitambulisha kama zoezi la kawaida ambalo vijana wanaweza kujifunza. Kutengeneza 'jukwaa' pamoja ni hatua nzuri, hivyo vijana wanaweza kuandaa mazingira mazuri ya kufanya mazoezi. Hii inafanya hali hiyo iwe ya kweli zaidi na haifai kulazimishwa. Ivute hewa ndani na kuitoa nje, kaa kimya baada ya zoezi na kutoa maoni ya kujenga ni mambo muhimu ya kuzingatia. Daima anza na kumaliza na maoni mazuri. Katikati unaweza daima kutoa mapendekezo ya kuboresha. Usitoe mapendekezo mengi ya kuboresha, kwa kuwa kutoa marekebisho mengi itafanya mshiriki kufikiri kwamba yeye hakufanya chochote kizuri kabisa. Kuwa mkali wakati unapouliza 'Amefanya nini vizuri?'. Na jibu liwe tu na maoni hasi. Waambie vijana kwamba maoni mabaya ya kujenga yatakuwa na wasiwasi baadaye na kwamba hivi sasa kila kitu ambacho kinaonekana kuwa bora ni kilichoenda vizuri.

# 4.16 KUWAKUTANISHA WATU WAWILI PAMOJA

**Lengo**
Vijana waendeleze mbinu na kufanyia zoezi ya namna ya watu wawili kutambulishana wao kwa wao. Waunde karatasi ya zoezi kwa hatua na vidokezo. Wafanyie zoezi mbinu.

**Maandalizi**
Angalia mwenyewe jinsi utakavyojibu maswali matatu hapa chini. Labda unaweza kutoa dondoo au vichwa vya habari kwa aya katika karatasi, lakini hakikisha huendi kuendeleza karatasi yote. Kikubwa ni kuruhusu vijana kuendeleza mbinu ya utendaji wenyewe na kuitumia katika onesho mbinu. Hakikisha una karatasi kubwa za kutundika na baadhi ya kalamu za wino mzito za kijani.

**Maelezo**
'Kwa sababu karibu kila mtu anaona kuwa ni ya kusisimua kidogo au inaogopesha kukutana na watu wapya, unaweza kuwa wa msaada. Wakati mwingine unajua mtu ambaye mtu mwingine anataka kuwasiliana naye. Unaweza kumsaidia mtu huyo kuwasiliana na mwingine. Wakati mwingine kwa njia nyingine; unataka kukutana na mtu ambaye tayari anajulikana kwa mtu unayemjua. Hivyo, unaweza kumwomba mtu huyo kukupeleka kwa mtu unayetaka kukutana naye. Leo tunaenda kuboresha njia yenye ufanisi kwa kumtambulisha mtu na tutaifanyia mazoezi.'

**Utendaji**
1 Baada ya kutambulisha somo, washiriki wataendeleza kubuni mbinu bora pamoja kama kundi, kwa kuzingatia maswali yafuatayo:
   - Kwanini unataka watu wajitambulishe kwa wengine?
   - Jambo gani muhimu kujua wakati wa kutambulisha watu kwa kila mmoja?
   - Ni hatua gani unayochukua wakati unataka watu wajitambulishe kwa wengine?
2 Waache vijana wafikiri juu ya maswali katika makundi ya watu wanne na waache waandike majibu yao kwenye karatasi ya zoezi au karatasi kubwa.
3 Waagize vijana kuning'iniza karatasi zao juu ya ukuta. Waweke alama ya kijani kwa kila karatasi.
4 Waache washiriki watembee kwenye chumba na kuzijadili karatasi za kila mmoja. Wanaweza kuziwekea alama hoja ambazo ni nzuri kwa mujibu wao.
5 Kisha, kila mtu anakaa tena katika makundi madogo. Kila kundi liandike muhtasari wa majibu mazuri juu ya maswali matatu kwenye karatasi mpya. Waelekeze waandae karatasi ya zoezi namba 4.16 'Kumsaidia mtu mwingine kukutana na mtu mpya'. 'Nadharia' yao jinsi ya kutenda kwa ufanisi zaidi.
6 Jadili ufupisho na rasimu katika kundi zima na muurekebishe kuuweka kwenye karatasi ya zoezi namba 4.16 'Kumsaidia mtu mwingine kukutana na mtu mpya'. Hili bado ni toleo la rasimu. Wakati karatasi ya rasimu itakapokuwa tayari, unaweza kulianza igizo 'kuwatambulisha watu kwa kila mmoja'. Karibisha washiriki watatu kufanya igizo mbele ya kundi zima.
7 Fafanua zoezi na majukumu tofauti kwa kutumia karatasi ya rasimu 4.16 'Kumsaidia mtu mwingine kukutana na mtu mpya':
   - Ni nani atakayetambulishwa kwa nani? Na nani? Kwanini?
   - Hali ikoje? Ni hali gani watu hawa wanayo?
   - Ni nani kwao huyu atakayetambulisha watu wawili kufahamiana?
   - Ni hatua gani zitakazofanyika? Je, utambulisho wake ukoje?
8 Wakati maandalizi yamefanywa, igizo linaweza kuanza na washiriki wengine wote ni watazamaji.
9 Baada ya hapo, kwanza waulize washiriki watatu wa onesho jinsi wanavyofikiri walifanya. Waache kwa sababu inaweza kuwa na kusababisha hofu kufanya zoezi hili mbele ya kundi zima.
10 Baada ya hayo unawauliza watazamaji yale waliyoyaona na yaliyokwenda sawia kwa mujibu wao. Je, kuna mapendekezo yoyote ya kuboresha? Ongeza maoni mazuri ikiwa inahitajika. Kisha unawashukuru washiriki waliofanya igizo kwa mchango wao na kuwaonesha shukrani yako kwa kuwa na ujasiri kufanya zoezi mbele ya kundi zima.
11 Jadili na kundi zima ikiwa kuna haja yoyote ya kuboresha rasimu ya karatasi ya zoezi kwa mujibu wa zoezi. Ikiwa ndivyo, uiboresha au uiongeze.
12 Uliza ambaye anataka kuchapa karatasi katika karatasi nzuri ya zoezi namba 4.16 'Kumsaidia mtu mwingine kukutana na mtu mpya'. Hili ndiyo toleo la mwisho.

**Tafakuri**
Waulize vijana jinsi walivyoiona njia hii ya kujifunza. Ilikuwaje katika kuibua nadharia wao wenyewe? Je, ni mambo gani wanaondoka nayo ili kuwatambulisha watu wawili kwa kila mmoja waliokuwa hawafahamiani katika maisha halisi? Ruhusu kila mmoja ataje angalau jambo moja.

***Dondoo***
Kuibua nadharia yako yenyewe huhamasisha, hasa wakati mchakato wa kufikiri matokeo unaingia rasmi katika karatasi ya kazi. Ni nadharia ya utendaji na ndogo, inayotokana na uzoefu katika maisha ya kila siku na kutafakari juu ya hili. Wakati karatasi ya rasimu ya kazi iko tayari, kikundi kinaweza kutafakari mara moja juu yake kwa kutumia nadharia hii katika onesho. Ikiwa kuna muda wa kutosha, unaweza kuamua kufanya zoezi la kuigiza katika vikundi vya watu wanne baada ya hatua ya 10. Washiriki watatu wanahitajika kwa ajili ya kuigiza na mmoja wao ni mtazamaji na mwingine ni mtunza muda. Badilisha majukumu wakati zoezi hilo limeisha. Waagize vijana kuitazama kwa umakini karatasi ya rasimu ya kazi na uulize kama uboreshaji unahitajika. Ikiwa ndivyo, uiboresha au uiongeze.

# 4.17

# JE, MTANDAO WANGU WA 'ULIMWENGU WA KAZI' UNAONEKANAJE?

**Lengo**
Vijana watoe hisia za mtandao wao wa 'Ulimwengu wa Kazi' na kuwa na ufahamu wa jinsi mtandao wao unavyokua au unavyoweza kukua.

**Maandalizi**
Fanya zoezi hili mwenyewe; mawazo yako yanaweza kutumika kama mfano kwa vijana. Na wewe pia unakuwa tayari kujibu maswali. Hakikisha una mtandao wa shule kuonesha taasisi zote na makampuni ambayo yameunganishwa nayo kwa ukaribu. Panga chumba katika hali ambayo vijana wanaweza kuzibandika karatasi zao kwenye ukuta na wanaweza kuzunguka ndani ya chumba. Hakikisha kuna karatasi kubwa za kutosha, kalamu za wino mzito na gundi ya karatasi.

**Maelezo**
'Kitu kikubwa cha mtandao ni kwamba kila mtu anao mmoja. Pia katika 'Ulimwengu wa Kazi'. Una mtandao hata kama mtandao huo ni mdogo au mkubwa, imara au dhaifu. Na jambo jema kuhusu hilo, ni kwamba unaweza kuutumia mtandao huo kwa njia nyingi. Ili kuonesha jinsi mtandao wako ulivyo au unaweza kukua, unaenda kuuchora mtandao wako kupitia sura ya ramani katika akili (mindmap).'

**Utendaji**
1. Acha washiriki waandike jina lao katikati ya karatasi.
2. Kisha waelekeze waongeze aina zote ambazo ziko katika 'Ulimwengu wa Kazi' kama makampuni, taasisi, mashirika na makundi mengine. Pia orodhesha aina ya wafanyakazi au kazi/vyeo vinavyounda kundi hili. Kwa mfano, kampuni ya ushirika na viongozi, wasimamizi, jamaa, wateja, n.k. Au makampuni na kazi, wamezisikia kupitia kwa wazazi, familia, kazi za muda au matembezi. Wanaweza pia kutumia mtandao wa shule kama mfano. Weka mzunguko mkubwa kuzunguka kila aina na uandike aina ya wafanyakazi ambao huunda kundi hili katika mduara huu.
3. Kwa makundi tofauti, washiriki waandike angalau majina mawili ya watu wanaowajua kuwa ni wa kundi hilo.
4. Ruhusu washiriki kubandika karatasi zao ukutani, ili waweze kuangalia na kuuzungumzia mtandao wa kila mmoja. Waelekeze kutafakari kama mtandao wao unahitaji kukua na kuwauliza ikiwa wanataka kuurekebisha mtandao wao baada ya kuona mitandao ya wenzao.
5. Waache washiriki kuchukua/kupiga picha ya mtandao wao wa 'Ulimwengu wa Kazi', ili mara zote waweze kuuangalia.

**Tafakuri**
Waulize washiriki ni nini waligundua wakati wa kufanya zoezi hili. Ni mawazo mapya yapi waliyoyaona kwenye karatasi za wanafunzi wenzao? Waliongeza nini baada ya kutazama mtandao wa washiriki wengine?

***Dondoo***

Zoezi hili la 4.17 ni sawa na zoezi la 4.3 'Je, mtandao wangu unaonekanaje? Katika 4.3 msisitizo ni juu ya aina zote za uhusiano - wote binafsi na mtaalamu - na katika 4.17 lengo ni kwenye uhusiano wa mtandao katika 'Ulimwengu wa Kazi'. Inawezekana kuwa washiriki wanafanya kazi kwa kampuni ndogo au mtu mmoja. Kisha uwaulize washiriki hawa jinsi gani ambavyo wangependa kuupanua mtandao wao, kwa mfano, na watu wanaowajua na wanaofanya kazi katika sekta hiyo. Au watu wanaowajua ambao walifanya mazoezi ya kazi yao katika kampuni moja, au watu wanaowajua kwa sababu walikuwa wateja wa kampuni hiyo. Kwa njia hii, wanaweza kupanua mtandao wao karibu na kampuni ndogo.

# 4.18

# JINSI NINAVYOUTUMIA MTANDAO WANGU WA 'ULIMWENGU WA KAZI'

**Lengo**
Vijana wachunguze kitu ambacho mtandao wao unaweza kuwafanyia. Wapange shughuli muhimu ili kuupata msaada wanaoutaka.

**Maandalizi**
Zipange meza kwenye chumba katika hali ambayo washiriki wanaweza kufanya kazi kwa urahisi kwenye karatasi za A3. Hakikisha una kalamu za wino mzito za kutosha na penseli.

**Maelezo**
'Jambo muhimu zaidi kuhusu mtandao wako ni, kiukweli, kuwa na ufahamu wa ukweli kuna watu wote walio karibu nawe ambao unaweza kuomba msaada kuhusu masuala mengi tofauti. Kwa upande mwingine, mawasiliano yako pia yanaweza kukuomba msaada. Ukubwa na uimara wa mtandao wako ulivyo, ndiyo msaada zaidi unaweza kuuomba ukakupa. Katika zoezi hili, tutakwenda kuchunguza kile mtandao wako unaweza kukuelezea wakati una swali kuhusu kazi, kazi yako ya baadaye au kazi ya sasa.'

**Utendaji**
1 Waulize washiriki wanachotaka kufikia, kulingana na uzoefu kutokana na kazi ndogo walizokuwa nazo, mazoezi yao ya utendaji au kazi wanayotaka kupata. Waambie waelezee lengo lao kwa umahusus kadri iwezekanavyo, ili washiriki wengine waweze pia kuunda wazo hilo.
2 Waache wajadili malengo yao katika makundi ya watu wawili na waache waboreshe mambo pale inapohitajika kupata maelezo mazuri na ya wazi, waache kwanza watengeneze rasimu ya maelezo.
3 Wape washiriki karatasi, penseli na kalamu za wino mzito 'markers'.
4 Waombe wachore duara na lengo lao liwekwe katikati. Anza sentensi na: 'Nataka ...'.
5 Waelekeze kufikiri ni watu gani katika mtandao wao wanaweza kuwa na msaada ili kufikia lengo hilo. Wanaweza kutumia mtandao ambao wamekuta katika zoezi la 4.3 'Je, mtandao wangu unaonekanaje?' au zoezi 4.17 'Mtandao wangu wa 'Ulimwengu wa Kazi' umeonekanaje?'
6 Waache washiriki waandike majina ya watu hawa kuzunguka duara. Majina ya mawasiliano ambayo ni muhimu sana yanaandikwe karibu na mduara, wale watu ambao wanatarajia msaada mdogo waandikwe mbali na mduara.
7 Waombe washiriki kuangalia kwenye majina ya watu waliyoandika. Wanawezaje kujihakikishia kwamba watu hawa watawasaidia? Kwa mfano: kuwapigia simu, kuwatembelea, kumuomba mtu wa kati kuwasiliana nao, kuwatumia barua pepe?
8 Waache washiriki kuongeza kwa kila jina jinsi watakavyowasiliana na mtu huyo.
9 Waombe washiriki kuandika mambo mahususi mawili ambayo wanaenda kuyafanyia kazi katika wiki mbili zijazo: vitu vinavyopaswa kuwa sawa na suala la jinsi ya kupata msaada kutoka katika mtandao wao kufikia malengo yao.
10 Panga tarehe ya kujadili zoezi hili, ili uweze kuangalia jinsi gani washiriki wote wamefanya shughuli zao za mtandao.

**Tafakuri**
Waulize washiriki wanavyojisikia kuhusu njia hii ya kuangalia mtandao wao. Je, waliweza kuweka malengo na hatua maalum ili kufikia lengo lao? Waulize washiriki kadhaa hatua watakazo chukua na watie moyo kundi zima kuhusika katika utendaji. Katika kipindi kingine, utekelezaji wa mpango mkakati ungeweza kufafanuliwa. Waulize vijana kile walichopata. Ni hatua gani ambazo wamechukua katika ulimwengu halisi? Ni mambo gani mazuri walikutana nayo? Je, ni mambo gani hasi waliyopata? Jinsi gani waliyatatua haya? Je, wamefanikiwa katika malengo waliyoweka? Je, wanapanga kufanya nini wakati hawajalifikia lengo lao?

***Dondoo***

Kuhakikisha kuwa washiriki wote watafikia lengo lao, inaweza kuwa muhimu kwamba wachache wao wanapaswa kuchukua hatua tena. Kujifunza jinsi ya kufanya mtandao, wakati mwingine huchukua muda mrefu kuliko inavyotarajiwa na huwezi kupanga kila kitu kwa mara moja. Hakikisha kuwa malengo yaliyowekwa yanafaa na yanaweza kuwa dhahiri kwao wenyewe. Lengo ambalo halijapangwa vyema, ndivyo litakavyokuwa gumu kuwasaidia watu katika mtandao wao. Unda kundi la mijadala ili wewe na kundi lako muweze kutiana moyo kufanya zoezi na kutoa vidokezo kwa kila mmoja.

4.19

# ORODHA YA MATAKWA YA MTANDAO WANGU WA 'ULIMWENGU WA KAZI'

**Lengo**
Vijana watengeneze orodha ya matakwa kuhusu kile wanachotaka kufikia kuhusiana na kazi yao kwa kutumia mtandao wao wa 'Ulimwengu wa Kazi'. Wapange shughuli ili kupata msaada wanaotaka.

**Maandalizi**
Itafaa kuandaa kabla malengo au matamanio ambayo vijana wanaweza kuongeza kwenye orodha yao ya matakwa. Fikiria: Kutafakari taarifa kuhusu taaluma fulani, kuzungumza na mtu fulani kutoka katika kampuni yao ya mafunzo kwa utendaji, kuzungumza na mshiriki wa zamani ambaye anafanya kazi katika kampuni hiyo, kutumia siku nzima na msimamizi wa kampuni au na mfanyakazi mwenye nafasi tofauti kabisa, kupata nafasi ya kuzungumza na msimamizi wa kampuni hiyo, kuhojiana na mtu fulani kutoka kwenye kampuni.

**Maelezo**
'Ukitaka kuwa na kazi inayokufaa, huenda ukataka pia kujua kila kitu kuhusu taaluma hii. Umevutiwa tu na kuhamasishwa! Katika zoezi hili, tunaenda kufanyia kazi hili kwa kuanzisha kile kinachoitwa 'orodha ya mtandao ya matakwa'. Unaweza kunuia chochote unachotaka; hiyo ndiyo sehemu bora ya orodha ya matakwa. Lakini ni juu ya mwingine kuamua ikiwa yeye anataka kuishi kulingana na matakwa yako.'

**Utendaji**
1. Waelekeze washiriki kuandika kile ambacho ni matakwa ya mtandao wao. Wanachofikiri juu ya kile wanachotaka kufikia kwa kutumia mtandao wao wa 'Ulimwengu wa Kazi' na wanaamua ni watu gani wanataka kuzungumza nao. Wape baadhi ya mifano kama itakapolazimu, lakini hakikisha wanajifikiria wenyewe. Waache wanong'one au wazungumze katika jozi.
2. Washiriki watakapokuwa wameandika matakwa ya mtandao wao, waulize maelezo zaidi watakayoomba ili wapate wanachotaka. Waache waandike angalau maswali matatu.
3. Weka washiriki pamoja katika makundi ya watu wanne na waache wajadili orodha yao ya matakwa yao kwa watu wa mtandao wa 'Ulimwengu wao wa Kazi'. Waombee kutoa vidokezo vingine kwa kila mmoja, akifafanua kile wanachotaka kutoka kwa kampuni ya mazoezi ya vitendo (internship).
4. Ninamjua nani? (unda matakwa yako) au, Ni nani ninayemjua anayemjua mtu ambaye? (unda msaada unaotaka) au, Ninamjua nani aliyefanya? (kuunda hatua).
5. Ahidiana na washiriki ni lini watamwendea angalau mtu mmoja kumwomba kitu kutoka katika orodha ya mtandao wa matakwa yako. Weka tarehe ambapo washiriki watapeana mrejesho kila mmoja kwenye yale waliyoyafanya na kubadilishana mawazo jinsi shughuli zilivyoenda.

**Tafakuri**
Waulize vijana walivyojiskia kuhusu zoezi hili. Waulize washiriki kadhaa waliyoandika kwenye orodha yao ya matakwa ya mtandao na nini watafanya. Waulize kama wanahitaji mwongozo wowote wa kuweka mpango wao katika utekelezaji. Katika darasa linalofuata, unajadili matokeo ya kazi ya nyumbani. Waulize washiriki ni nini waliyofanikiwa kufanya katika baadhi ya vipengele vya orodha yao ya mtandao wa matakwa. Je, walifikia kile walichokitaka? Je, wamekuwa wenye hekima? Je, kuna vidokezo vya vitendo vya kufuatilia?

***Dondoo***

Wahimize vijana wasifikiri mara moja kuwa malengo yao hayawezekani; daima wanaweza wakayafuta baadaye. Wahimize kufanya matakwa yao wazi. Kwa njia hii wanaweza kujifunza zaidi kuhusu wao wenyewe na huwasaidia kuchunguza ikiwa matakwa yao kama ni ya kweli.
Inawezekana kuwa vijana hufanya kazi kwenye kampuni ndogo au kampuni ya mtu mmoja. Hivyo itakuwa ngumu kutambua matakwa yao. Katika hali hiyo, mtu kutoka kampuni hiyo amsaidie mshiriki kupata kampuni nyingine (wenzake) kuzungumza kuhusu swali moja au mawili kutoka kwenye orodha yao ya matakwa. Kwa njia hii, mshiriki anaweza kutumia kampuni yake kama hatua ya kupanua mtandao wake.

## 4.20

# KASI YA MAHUSIANO: MAZUNGUMZO NA WENZA WA SHULE NISIOWAJUA

**Lengo**
Vijana wawe na mazungumzo na wenzao ambao hawawajui.

**Maandalizi**
Kwa zoezi hili, ni muhimu kuwaleta pamoja vijana kutoka kwenye makundi tofauti ya mafunzo. Kimsingi, vijana hawa hawafahamiani. Panga viti bila meza kwenye chumba katika hali ambayo vijana wanaweza kuzungumza kwa makundi ya watu wawili.

**Maelezo**
'Katika maisha yako yote, unazungumza na watu usiowajua. Hii inaweza kuwa majadiliano madogo, kwa mfano kwenye soko au katika duka. Na ingawa tunafanya hivyo mara nyingi, si rahisi kila wakati. Hata hivyo, ni muhimu kujifunza kuzungumza na watu usiowajua, kwa kuwa na mazungumzo na wageni unapata vitu ambavyo hujawahi kupata kujifunza vinginevyo. Unakutana na watu ambao wanaweza kuwa marafiki zako mwishoni. Au unawajua watu ambao wanaweza kuwa na manufaa kwako kuhusiana na maendeleo yako ya kazi. Katika zoezi hili, tutazungumzia kuhusu kozi tofauti za mafunzo tunayojifunza.'

**Utendaji**
1 Waweke washiriki ambao hawajuani pamoja wakiwa wawili.
2 Waache wawe na majadiliano kuhusu mafunzo yao.
3 Mazungumzo haya yaendelee kwa dakika 7, kwa kiwango cha juu.
4 Kisha muelekeze mshiriki mmoja kuhamia kwa mshiriki mwingine ambaye hawajuani.
5 Kisha mazungumzo mapya yaanze tena.
6 Zoezi hili liishe baada ya kubadilisha maeneo ya ushiriki mara 5.

**Tafakuri**
Je, waliionaje namna ya kubadilishana uzoefu na mshiriki ambaye hawajuani? Je, ni maswali gani ya kuvutia/maalumu/ya kushangaza? Je, vijana walijifunza nini ambacho hawakuwa wakifahamu kabla? Je, kuna mtu yeyote anayetaka kuuliza swali la mwisho?

***Dondoo***
Waambie vijana kwamba wanaweza kuuliza kitu chochote kinachokuja katika akili zao. Kama mtu mwingine hataki kujibu swali fulani, atasema jambo hili. Hii itahusu kuwa na mazungumzo juu ya mawazo ambayo kila mtu anayo kuhusu mafunzo yao. Kuna vikwazo tu kadri muda unavyohusika, si katika maudhui.

**Uchunguzi wa kina**
Bila shaka, inawezekana pia kutoa zoezi kwa ajili ya kuanza mazungumzo na vijana wengine watatu wasiofahamiana na wapo katika mafunzo tofauti. Hii inaweza kuwa rahisi wakati wa mapumuziko. Hii inahitaji mipango zaidi na ujasiri wa mshiriki. Weka miadi wakati utapoenda kujadili zoezi hili.

4.21

# KASI YA MAHUSIANO: MAZUNGUMZO MACHACHE NA WATU NISIOWAJUA

KARATASI YA ZOEZI 4.21

**Lengo**
Vijana wajifunze wenyewe katika kuzungumza na watu ambao hawajui bila kuamua kabla juu ya mada itakayozungumziwa.

**Maandalizi**
Fikiria kabla, jinsi unavyotaka kulijadili zoezi hili na washiriki baada ya kuzungumza na mtu ambaye hawafahamiani nae. Ni kwa namna gani unataka washiriki kushirikishana uzoefu wao na kundi zima? Kuna njia mbalimbali za kufanya hivyo. Kwa mfano, unaweza kuwaelekeza washiriki kujipiga picha na watu wale ambao waliongea nao. Au uwaelekeze kuandika dondoo muhimu ambazo zinaelezea kuhusu uzoefu wao. Uwezekano mwingine ni kuwaelekeza washiriki kuchora mchoro wa yale waliyoyaona katika mazungumzo. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 4.21 'Jinsi ya kuwa kinara katika mazungumzo mafupi?'

**Maelezo**
'Tunaposema kuhusu ‘mazungumzo mafupi', tunataja jambo ambalo watu wanasema tu kuhusu' hii, hiyo na nyingine’. Inaonekana mazungumzo juu ya mambo yasiyo ya maana. Lakini ni kweli? Kuwa na majadiliano madogo ni muhimu sana. Kwa sababu kwa njia hii unafanya uhusiano na watu walio karibu nawe. Unaweza kutumia aina hii ya mazungumzo ili kukutana na watu wapya, kuboresha uhusiano uliopo au kujifurahisha tu. Unapoanza mazungumzo, huenda usizungumze mara moja juu ya magonjwa yako au matatizo ya kibinafsi. Anza kwa makini na unapata hisia unayoweza kuzungumza na mtu huyo. Katika zoezi hili, tutazungumza na wageni mitaani, dukani au popote.'

**Utendaji**
1 Fafanua kwa pamoja kuhusu desturi zipi za 'mazungumzo mafupi' zilizopo Tanzania. Unaweza kufanya nini unapokutana na wageni mitaani, dukani au kwenye kampuni? Na ni nini kisichofaa kufanya?
2 Wape karatasi ya zoezi 4.21 'Jinsi ya kuwa kinara katika mazungumzo mafupi?’ Waache washiriki wasome karatasi na waache wajadiliane katika makundi ya watu watatu. Je, kuna maelekezo ya kutoa ambayo yanahusishwa na kaida za salamu za Tanzania? Je, kuna taratibu juu ya kile ambacho huwezi kufanya, kwa sababu ni kibaya?
3 Yajadili matokeo ya vikundi na taratibu zinazojitokeza.
4 Wape washiriki kazi ya kufanya katika wiki ijayo (au wiki mbili) katika maeneo kadhaa. Suala la maana sio unaloliongea, lakini ukweli ni kwamba unaongea na watu usiowajua.
5 Panga tarehe unapotafakari juu ya zoezi hili.
6 Katika mkutano ujao, washiriki washirikishane uzoefu wao na kundi zima. Katika maandalizi yako umeamua jinsi ya kufanya hivyo.

**Tafakuri**
Uliza, katika mkutano ujao, jinsi washiriki walivyoona namna ya kukutana na wageni mitaani na kuanza mazungumzo nao? Je, walipata shida gani? Walipata urahisi gani? Je, iliwezekanaje kukutana na wageni na kuanza mazungumzo nao? Waliona kipi kilichokuwa kizuri? Waliona kipi kisichokuwa kizuri? Je, walifanya zoezi peke yao au walifanya hivyo pamoja na washiriki wengine? Walijifunza nini kutokana na zoezi hili?

***Dondoo***
Hakikisha unakuwa makini na mila ya salamu na misemo midogo ya kawaida ya maongezi ya Tanzania. Pia, fikiria taratibu unazoweza kuwapa washiriki, hivyo unaweza kuwasaidia kuandaa kazi.

# KARATASI YA ZOEZI 4.4.1



**Maelekezo ya jumla**

1 Kwanza, andika makundi yote ya watu unayoyafahamu kwenye karatasi inayojitegemea. Fikiria kuhusu familia yako, marafiki, majirani, wanafunzi wenzako, jamaa zako n.k.

2 Kisha, chukua karatasi ya A3 na chora mtandao wako. Tumia pia mawasiliano ya namba za simu ulizonazo kwenye simu yako na barua pepe yako. Weka alama ya nukta kwa kila mtu mmoja kwenye karatasi na andika jina mbele yake. Utachora mstari baina yako (katikati) na watu unaowafahamu. Pia utachora mstari baina ya watu ambao unadhani wanafahamiana. Mstari unaonesha kuwa kuna uhusiano baina yako na watu wa mtandao wako na pia baina yao.

**Chora mtandao wako**

3 Anza na wewe mwenyewe, weka nukta moja na jina lako.

4 Weka nukta ya pili na karibu yake andika jina la mmoja wa watu mnaowasiliana. Chora mstari baina yako na mtu huyo.

5 Fikiria kuhusu mtu ambaye nyote mnamfahamu.

6 Chora nukta kwa ajili ya mtu huyu pia na andika jina lake karibu na nukta hiyo. Chora mstari baina yako na mtu huyu, na pia mstari baina ya mtu huyu na watu wengineambao wote mnawafahamu.

7 Andika jina la mtu mwingine unaemfahamu kisha endelea.

8 Rudia hatua ya 4, 5, 6 na ya 7 mpaka utakapomaliza kujaza mawasiliano uliyonayo kwenye makundi yote uliyoorodhesha kwenye hatua ya kwanza.

9 Kaa chini na tazama mtandao wako.

10 Chora duara za rangi tofauti kuzunguka majina yote ya kwenye kundi moja.

**Jibu maswali yafuatayo**

11 Kuna makundi mangapi yaliyopo katika mchoro wa mtandao wako (kuna rangi ngapi tofauti)?

12 Makundi haya tofauti yana tabia zipi?

13 Kundi gani lina watu wengi zaidi?

14 Kundi gani lina mistari iliyoungana zaidi na makundi mengine?

15 Kundi gani lina mistari michache zaidi iliyoungana na makundi mengine?

16 Je, kuna watu ambao wana mahusiano na wewe tu na hawana uhusiano na kundi lako lolote?

# KARATASI YA ZOEZI 4.4.2

**Jibu maswali yafuatayo katika jozi:**

- Kitu gani kilichokushangaza katika mchoro wa mtandao wako?

- Kitu gani kilichokushangaza katika mtandao wa wanakikundi wenzako?

- Mtandao wako una watu wangapi?

- Hawa ndio watu wote unaowafahamu?



# KUUCHANGANUA MTANDAO WANGU



- Watu uliopanga kwenye kundi moja (rangi moja) wana tabia gani zinazofanana? Bainisha kwa kila rangi ni ipi sifa hii:

- Kitu gani cha ziada ambacho watu wenye rangi moja wanafanana?

- Ni kwa watu gani kutoka kwenye mtandao wako unapata msaada zaidi?

# KARATASI YA ZOEZI 4.5.1

**Uhusiano imara: uhusiano wa karibu au marafiki**
Uhusiano wa karibu ni kama kuwa na marafiki wazuri. Wao ndio hukujali vya kutosha na hukuchukulia vile ulivyo. Wako tayari kukusaidia wakati wowote. Inahitaji muda na uaminifu kujenga uhusiano imara. Hii inaendana zaidi na watu ambao mnafanana katika mambo mengi. Uhusiano imara huwa ni muhimu zaidi pale unapohitaji kutambulishwa kwa mtu fulani au pale unapohitaji kuongelea jambo la siri.

**Uhusiano dhaifu: watu wa mbali au jamaa**
Watu wa mbali au jamaa ni watu ambao mnashirikiana mambo machache. Wanafahamu kidogo malengo yako na wewe ni nani. Mnakutana kwa miadi tu. Mnabadilishana msaada. Ukimsaidia mtu huyu unategemea kitu fulani akurudishie siku zijazo. Ingawa watu hawa wa mbali ni msaada kwa maendeleo ya fani yako. Mara nyingi wanakuwa na mtazamo tofauti wa mambo zaidi yako. Wanakukutanisha na watu ambao usingeweza kukutana nao mwenyewe. Wakati unapotafuta fursa mpya, unaweza kufaidisha watu wengi ambao sio kama wewe.

Andika kwenye jedwali majina ya watu unaowafahamu. Hapa, tunamaanisha watu mnaofahamiana. Labda unamfahamu muimbaji maarufu. Je, na yeye anakufahamu pia na huwa mnasalimiana anapokuwa anapiga muziki? Ndio? Hivyo andika jina la mwimbaji huyo. Hapana? Basi usiandike jina la mwimbaji huyo.

Kwanza jaza kwenye safu majina, namna mnavyofahamiana na taaluma. Unaweza kuirefusha orodha hii kadri utakavyo kwa kuorodhesha watu wote unaowafahamu.

Baada yakuwa umejaza safu Uhusiano: imara au dhaifu. Uhusiano imara unamaanisha mtu huyo unamfahamu vizuri sana. Uhusiano dhaifu maana yake unamfahamu mtu huyo kwa kiasi kidogo.



# MTANDAO WANGU, KAZI NA NGUVU YA UHUSIANO

**Maana ya 'dhaifu' (= kidogo) na 'imara' (= vizuri):**

- 'dhaifu: kidogo' maana yake umemuona mtu huyu mara nyingi, na kwa mfano, unamfahamu mtu huyu kutokea mbali na mara nyingi mmekuwa mkikutana katika mazingira rasmi. Cha msingi ni kutambua kuwa watu hawa wana ujamaa.

- 'imara: vizuri' maana yake umekuwa ukimuona mtu huyu mara kwa mara na kwa mfano, unafahamu kuwa mtu huyu ana dada wawili na anapendelea muziki gani. Mara kwa mara mmekuwa mnatoka pamoja. Mnaaminiana na hamuogopi kuelezana jambo lolote.

# KARATASI YA ZOEZI 4.5.1



| | JINA | MNAFAHAMIANA VIPI? | TAALUMA | UHUSIANO 'IMARA' AU 'DHAIFU' |
|---|---|---|---|---|
| Mfano | Said Juma Ali | Baba | Seremala | Imara |
| Mfano | Aisha Khan | Jirani | Muuguzi | Dhaifu |
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |
| 11 | | | | |
| 12 | | | | |
| 13 | | | | |

Mtandao wako -kuonesha watu unaowafahamu- mara nyingi huonekana tofauti na wanakikundi wengine au mkufunzi wako. Na mara nyingi iko tofauti na mtandao wa jamaa zako.

Katika zoezi hili, utachora mtandao wako katika duara ukurasa unaofuatia.

Fuata hatua zifuatazo:

**Hatua ya 1**
Bila shaka, dunia haijagawanyika kwa uwazi kwenye mahusiano imara au dhaifu, au katika 'marafiki wazuri' na 'jamaa'. Mahusiano mengine yako kwa wakati.

a Andika kwenye duara jekundu watu unaowafahamu vizuri sana ('marafiki wazuri')
b Andika kenye duara la njano watu mnaofahamiana vizuri kwa sababu ('uso uliozoeleka')
c Andika kwenye duara la rangi ya chungwa watu mnaofahamiana kwa kiasi kidogo ('jamaa')

**Hatua ya 2**
Watu unaowafahamu, wanaweza kuwa wanafahamiana vizuri pia. Chora mstari baina ya watu ambao unadhaniwa nafahamiana nao.


**Hatua ya 3**
Sasa umeshachora mtandao wako binafsi. Kuna kitu kinakushangaza? Unaweza kufikiria mambo yafuatayo:

- Hapo kuna watu ambao wana uhusiano na wewe tu?
- Nani ambae ana uhusiano na watu wengi zaidi?
- Duara gani lina mistari mingi zaidi?





**Katika michoro yako onesha uimara na udhaifu wa mahusiano yako**



# KARATASI YA ZOEZI 4.6

# MFANANO NA UTOFAUTI KATIKA MTANDAO WANGU

MADA YA 4.6

Andika majina kumi (tofauti) ya watu kutoka kwenye mtandao wako katika jedwali lifuatalo: Kumbuka: usiorodheshe wanakikundi wenzako tu.

Sasa tafuta tabia mbili ulizonazo zinazofanana na hao watu kumi. Pia tafuta tofauti ulizonazo na watu hao. Kwa mantiki ipi unaweza kuzungumzia mfanano na utofauti?

Mbali na vile wewe mwenyewe unavyofanana na watu kwenye orodha yako, lazima iwe na kufanana kati yao fikiria kuhusu umri, taaluma, michezo n.k. Chora mistari baina ya tabia ambazo watu wa kwenye mtandao wako wanafananisha.

Jadili orodha yako ukiwa na jirani yako. Jibu maswali yafuatayo:

a Ni upi mfanano na utofauti baina ya watu waliopo katika mtandao wangu?

b Ninaweza kuwafuata watu hawa nikiwa na aina gani ya maswali kuhusu maendeleo ya fani yangu?

c Je, ninawafahamu watu wakutosha wenye tabia tofauti ambao wanaweza kunisaidia katika maendeleo ya fani yangu? Naweza kuhitimisha vipi?

| | Jina | Umri | Ninamfahamu vipi? | Me/ ke | Mfanano | Mfanano | Utofauti | Utofauti |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | | |
| 4 | | | | | | | | |
| 5 | | | | | | | | |
| 6 | | | | | | | | |
| 7 | | | | | | | | |
| 8 | | | | | | | | |
| 9 | | | | | | | | |
| 10 | | | | | | | | |

# KARATASI YA ZOEZI 4.7.1

# TAALUMA WALIZONAZO WATU KATIKA MTANDAO WANGU

Je, unatambua taaluma walizonazo watu waliopo katika mtandao wako?
Andika majina na taaluma walizonazo watu unaowafahamu:

1 ____________________
2 ____________________
3 ____________________
4 ____________________
5 ____________________
6 ____________________
7 ____________________
8 ____________________
9 ____________________
10 ____________________
11 ____________________
12 ____________________
13 ____________________
14 ____________________



15 ____________________
16 ____________________
17 ____________________
18 ____________________
19 ____________________
20 ____________________
21 ____________________
22 ____________________
23 ____________________
24 ____________________
25 ____________________
26 ____________________
27 ____________________
28 ____________________
29 ____________________
30 ____________________

# KARATASI YA ZOEZI 4.7.1

# TAALUMA WALIZONAZO WATU KATIKA MTANDAO WANGU

MADA YA 4.7

**Jambo gani linanishangaza kuhusiana na taaluma walizonazo watu katika mtandao wangu?**
Kaa na tazama mtandao wako na taaluma walizonazo watu waliopo katika mtandao wako kwa umakini. Kuna taaluma nyingi tofauti tofauti? Je, kuna taarifa zinazokidhi sifa na shauku yako? Je, kuna taaluma ambazo zinakuvutia?

**Watu wawili wanaonivutia katika mtandao wangu.**
Kama ningelipendekeza watu wawili, ningechagua:

1 Jina______________________________

Ninaweza kwenda kwake kumuuliza kuhusu:___________________________

_______________________________________________________________________

Ninaweza kutumia msaada wake kuendeleza fani yangu kwa sababu yeye:

_______________________________________________________________________

2 Jina______________________________

Ninaweza kwenda kwake kumuuliza kuhusu: ___________________________

_______________________________________________________________________

Ninaweza kutumia msaada wake kuendeleza fani yangu kwa sababu yeye:

_______________________________________________________________________

# KARATASI YA ZOEZI 4.7.2

**Andaa orodha ya watu ambao wanaweza kuwa wa msaada kwa maendeleo ya fani yako.**
Wakati wa kipindi/darasa, unasikia watu wengi ambao wanaweza kukuvutia kwa sababu fulani. Watu hao hawapo kwenye mtandao wako, lakini wanauhusiano na mtu mwingine. Ni muhimu kuandaa orodha yao, labda unahitaji kuwasiliana na mmoja kati yao siku zijazo.

Andika majina yao, taaluma, wao ni mtandao wa nani na anaweza kutoa msaada gani?

1 Jina:

Taaluma:________________________________________

Kutoka katika mtandao wa:________________________________________

Mawasiliano:________________________________________

Naweza kumuomba msaada wa:

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________





2 Jina:

Taaluma:________________________________________

Kutoka katika mtandao wa:________________________________________

Mawasiliano:________________________________________

Naweza kumuomba msaada wa:

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

3 Jina:

Taaluma:________________________________________

Kutoka katika mtandao wa:________________________________________

Mawasiliano:________________________________________

Naweza kumuomba msaada wa:

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

# KARATASI YA ZOEZI 4.8.1

# MSAADA WANGU KWA WENGINE

Kumbuka mwezi uliopita. Nani ulimsaidia na kwa lipi? Hii inaweza kuwa chochote ulichosaidia!

**Niliwasaidia watu wafuatao:**

a. ______________________________

b. ______________________________

c. ______________________________

**Nilimsaidia:**

a. ______________________________

b. ______________________________

c. ______________________________

**Jibu maswali yafuatayo:**

- Unafahamu zaidi kuhusu nini?
- Kitu gani unaweza kufanya kwa ufasaha?
- Unamfahamu nani, hivyo nani unaweza kumkutanisha na mtu fulani?

**Ninafahamu zaidi kuhusu:**

______________________________

______________________________

______________________________

**Ninaweza kufanya kwa ufasaha::**

______________________________

______________________________

______________________________

**Ninafahamu watu wafuatao, ambao wanaweza kuwavutia wanakikundi wengine:**

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

# KARATASI YA ZOEZI 4.8.1

**Kazi ya nyumbani**
Mara nyingine ni ngumu kujisemea mambo ambayo wewe unayamudu. Hivyo, unapewa kazi ya kumuuliza mwingine akufafanulie hili. Unaweza kuchagua nani utamuomba akufanyie hili: kwamfano, wazazi wako, majirani zako, jamaa au rafiki ambae sio sehemu ya kundi hili.

Muache aoneshe mambo unayoyaweza kwenye orodha hapo chini (mambo unayoyajua sana), mambo ambayo unaweza kufanya kwa ufasaha na nani unaemfahamu. Unaweza kuomba watu kadhaa wakujazie orodha hiyo hapo chini.

(Jina lako) ______________________________unajua zaidi kuhusu:

______________________________

______________________________

______________________________

(Jina lako) ______________________________unaweza kufanya kwa ufasaha:

______________________________

______________________________

______________________________



# MSAADA WANGU KWA WENGINE



(Jina lako) ______________________ unafahamu watu wafuatao (ambao wanaweza kuwa na manufaa kwa wanakikundi wengine):

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

# KARATASI YA ZOEZI 4.8.2

**Andaa orodha ya watu ambao wanaweza kuwa msaada kwa maendeleo ya fani yako.**
Ukiwa darasani, unasikia watu wengi ambao wanaweza kuwa na manufaa kwako. Watu hao hawapo kwenye mtandao wako, lakini wana uhusiano na mtu mwingine. Ni muhimu kuandaa orodha yao, labda unahitaji kuwasiliana na mmoja kati yao siku zijazo.

Andika majina yao, taaluma, ni mtandao wa nani na anaweza kutoa msaada gani?

1 Jani:

Taaluma: ______________________________

Kutoka katika mtandao wa: ______________________________

Mawasiliano: ______________________________

Naweza kumuomba msaada wa:

______________________________

______________________________

______________________________



# WATU NINAOWEZA KUWAOMBA MSAADA

MADA YA 4.8

2 Jina:

Taaluma: ______________________________

Kutoka katika mtandao wa: ______________________________

Mawasiliano: ______________________________

Naweza kumuomba msaada wa:

______________________________

______________________________

______________________________

3 Jina:

Taaluma: ______________________________

Kutoka katika mtandao wa: ______________________________

Mawasiliano: ______________________________

Naweza kumuomba msaada wa:

______________________________

______________________________

______________________________

# KARATASI YA ZOEZI 4.9

**Kuandaa ombi la msaada**
Fikiria kuhusu swali ambalo unahitaji kuwauliza watu waliopo kwenye mtandao wako. Liwe linalohusu kazi unayotegemea kufanya, na mafunzo kazini au kazi ya muda ambayo unahitaji kupata. Unaweza pia kuamua kuomba ushauri kwa mtu kuhusu masuala kama vile: mambo gani unayaweza? Mambo gani unayaweza kidogo? Ni taaluma ipi inakufaa?

Ukiomba msaada vizuri zaidi na kwa uwazi, hivyo hivyo ndio utapata majibu! Hakikisha unafanya kwa ufupi na uwazi. Fikiria kuhusu vigezo ulivyounda na kikundi mwanzoni mwa kipindi. Anza swali lako na:

Ninahitaji mtu ambaye:



# NI MSAADA GANI NAWEZA KUUTUMIA

**Boresha maswali yenu katika jozi**
Swali linaweza kueleweka kabisa kwako, lakini hii haina maana kuwa wengine watakuelewa kabisa. Sasa mnaenda kuboresha maswali yenu, ili kila mmoja aelewe kitu unachohitaji naafikirie sawa na wewe.

Boresheni maswali yenu kwa kusikilizana kwa ukaribu. Unaelewa swali la mwanakikundi mwenzako na kinyume chake? Kama hapana, endelea kuuliza mpaka utakapoelewa kwa kina kileanachomaanisha. Tumia maswali ya wazi kama vile: kwanini unauliza hivi? Unamaanisha nini? Unaweza kufafanua nini......? Maswali yakiwa dhahiri na thabiti zaidi, ndivyo itakavyoleta wepesi kwa watu wengine kukusaidia.

Utakapokuwa na furaha juu ya swali lako, andika marekebisho yake hapo chini. Je, unaweza kufafanua kwanini unaliona bora swali hili?

Ninamtafuta mtu ambaye:

# KARATASI YA ZOEZI 4.9

**Nani katika mtandao wako anaeweza kukusaidia?**
Kumbuka: Inaweza kuwa watu ambao wanaweza kukusaidia moja kwa moja, lakini pia watu wanaoweza kukupatia maoni ya yupi uwasiliane nae.

| JINA | ANAWEZA KUNISAIDIA KWA LIPI? |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |



# NI MSAADA GANI NAWEZA KUUTUMIA

MADA YA 4.9

**Majibu niliyopata**
Andika mtu ambaye ulimuomba msaada na majibu uliyopata.

| JIBU | MAJIBU NILIYOPATA |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

# KARATASI YA ZOEZI 4.10

| Maelezo | Mara nyingine | Mara nyingi | Asilani |
|---|---|---|---|
| **1.** Ninaongea kwa urahisi na baadhi ya watu kuliko wengine | | | |
| **2.** Kama sijisikii huru na mtu fulani, inajidhihirisha katika vitendo vyangu | | | |
| **3.** Sipendi kuongelea mambo binafsi ninapoona watu nisiowafurahia | | | |
| **4.** Ninaendelea kusimulia hadithi yangu hata kama hakuna anaenisikiliza tena | | | |
| **5.** Ninawaacha wenginewamalizekuongea kabla sijaanza kuzungumza | | | |
| **6.** Ninaweza kutoa maelezo kwa urahisi kuhusu ninavyowaza na ninavyojisikia | | | |
| **7.** Huwa ninamuangalia mtu wakati ninapoongea nae | | | |
| **8.** Ninapokuwa sijaelewa kitu, huwa ninauliza kupata ufafanuzi | | | |



# MAELEZO KUHUSU NAMNA NINAVYOWASILIANA



| Maelezo | Mara nyingine | Mara nyingi | Asilani |
|---|---|---|---|
| **9.** Ninapomwambia kitu mtu fulani, ninakuwa makini kufahamu kama ananielewa | | | |
| **10.** Huwa nathubutu kutawala jukwaa kiurahisi, haijalishi ni mahali gani | | | |
| **11.** Ninasikiliza kwa umakini wakati mtu anapokuwa anaongea | | | |
| **12.** Ninatumia ishara kuonesha kuwa ninasikiliza | | | |
| **13.** Ninakuwa makini na ishara za mtu ambaye ninazungumza nae | | | |
| **14.** Ninaweza pia kumuelewa mtu hata asipozungumza | | | |
| **15.** Watu wanaponieleza kitu, ninawaeleza namna ninavyojisikia | | | |
| **16.** Mara nyingi mimi ndio sababu ya kukatisha mawasiliano | | | |

# KARATASI YA ZOEZI 4.13

# KUCHUNGUZA MAHUSIANO NA MAZUNGUMZO KWA MARA YA KWANZA

Ukiwa kama mtazamaji, andika kila kitu unachogundua kwa kufuatanisha maswali yafuatayo. Ni kitu gani mwanakikundi mwenzako hufanya pale anapoanzisha mazungumzo? Angalia kwa ukaribu yale anayosema na kufanya. Kuwa makini na yanayotokea na chukua nukuu ya yale ambayo yalienda vizuri na ambayo yangeenda vizuri. Toa maoni kwa ajili ya uboreshaji.

**Zoezi la 1**

Umegundua kitu gani?

Kitu gani kilienda vizuri mazungumzo hayo?

Kitu gani kingefanyika vizuri zaidi?

**Zoezi la 2**

Umegundua kitu gani?

Kitu gani kilienda vizuri kwenye mazungumzo hayo?

Kitu gani kingefanyika vizuri zaidi?

# KARATASI YA ZOEZI 4.13

**Zoezi la 3**
Umegundua kitu gani?

Kitu gani kilienda vizuri kwenye mazungumzo hayo?

Kitu gani kingefanyika vizuri zaidi?

**Baada ya zoezi, mwanakikundi mwenzako aelezee kwanza namna gani anadhani mazungumzo yamefanyika; kisha mtu ambaye alijaribu kuwasiliana nae aeleze namna gani mazungumzo yalikuwa, na hatimae utatoa mrejesho kama mtazamaji. Unaweza pia kutoa karatasi yako na mtazamo wako.**



# KUCHUNGUZA MAHUSIANO NA MAZUNGUMZO KWA MARA YA KWANZA

MADA YA 4.13

**Orodha ya mambo ya 'kufanya' na 'kutofanya'**

| Kufanya | Kutofanya |
| --- | --- |
| 1 | 1 |
| 2 | 2 |
| 3 | 3 |
| 4 | 4 |
| 5 | 5 |

# KARATASI YA ZOEZI 4.14

Fikiria kuhusu mtu ambae ni mwanamtandao halisi katika upeo wako. Huyu ni mtu ambaye hufanya mawasiliano kiurahisi na kila mara anafanya mawasiliano na anayefahamu namna ya kudumisha mawasiliano. Nani ambaye yuko makini sana kati ya marafiki na jamaa zako? Huyu anaweza kuwa mtu wa kwenye kituo cha redio au luninga, lakini pia anaweza kuwa mtu kutoka kwenye mtandao wako, mtu ambaye unamfahamu.

Andika hapo chini nani unamfikiria na kwanini unadhani ni mwanamtandao halisi. Fikiria hasa hasa yale anayofanya mtu fulani. Unaona au kusikia watu hawa wakifanya nini?

**Mwanamtandao halisi....**

Ninadhani ______________________________ni mwanamtandao halisi kwa sababu:

______________________________

**Ninafanya kitu gani ili kuendelea kuwa na mawasiliano na watu hawa?**

______________________________

______________________________

Mtu ambaye unadumisha mawasiliano nae atakukumbuka haraka sana. Hii inamaanisha mambo mawili. Mnawasiliana mara nyingi kwa sababu unampenda mtu huyo. Au unadumisha mawasiliano na mtu huyo kwa sababu anaweza kukusaidia siku zijazo.

Dumisha mawasiliano na hakikisha uhusiano wenu haufifii kadri muda unavyozidi kwenda, kwa sababu hii inawezakuwa ngumu kuwaomba msaada watu hawa. Hakikisha unakuwa karibu na watu hawa kwa kuonana kifikra. Ili, siku wakifahamu unahitaji nini, wawe tayari kukusaidia.



# MWANAMTANDAO HALISI...

**Kipi cha ziada ninachoweza kufanya?**
Kitu gani cha ziada ninachoweza kufanya ili kuendelea kuwasiliana na watu hawa?

______________________________

______________________________

______________________________

# KARATASI YA ZOEZI 4.14

# MWANAMTANDAO HALISI...



| Vitendo | Nina....kufanya hivyo (penda/chukia) | Mara ngapi? | Na nani? | Kwanini ndio au hapana? | Kuna faida gani? |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| **Kuongea kwa kutumia simu** | **Napenda ku** | **Mara nyingi** | **Mjomba Mohammed** | **Ana habari/masimulizi mazuri** | **Inafurahisha na ninajifunza kutoka kwake** |
| **Kutumiana barua pepe** | **Napenda ku** | **Mara nyingi** | **Msimamizi wangu wa mafunzo kazini, yaliyopita** | **Ni haraka na rahis** | **Anafahamu kitu ninachohitaji** |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

# KARATASI YA ZOEZI 4.15



1 Muangalie machoni mwenzako.

2 Nenda kwa mtu mwingine

3 Jitambulishe:
- Sema 'habari yako' na mpe mkono, kama inaruhusiwa kwenye utamaduni wenu. Mtazame mtu huyo kwa umakini;
- Taja jina lako;
- Sema kitu kuhusu wewe, kinachokushughulisha, nini shauku yako? Linaweza kuwa jambo lolote ilimradi litoe taarifa inayokuhusu.

4 Sikiliza kwa makini namna mtu huyo anavyojitambulisha:
- Hakikisha unakumbuka jina lake;
- Hakikisha unakumbuka kile anachozungumzia mwenzako na baadaye kizungumzie katika mazungumzo yenu.

**Hii ndio njia ya kufanya mazungumzo yaendelee:**

1 Sikiliza kwa makini yale anayokwambia mwenzako.

2 Uliza maswali ya wazi. Maswali ambayo huwezi kuyajibu kwa majibu ya ndiyo au hapana. Mawasiliano hufanyika kwa wepesi kwa kuuliza maswali ya wazi, mazingira ni safi na wazi, na utajua mengi kuhusu mwenzako. Maswali ya wazi mara nyingi huanza na viulizo: nani, nini, wapi, lini na jinsi (gani)?

3 Endelea kuuliza kuhusu taarifa zaidi ili kuelewa anachokwambia mtu huyo.

4 Hakikisha una 'vianzilishi vya mazungumzo' vya kutosha. Vianzilishi vya mazungumzo ni maswali au maneno ya kufungulia, kuanzisha mazungumzo. Haya ni maswali ambayo watu wanaweza kuyajibu kwa urahisi. Mfano ni maswali au maneno kuhusu mahali ulipo kuhusu jinsi wengine walivyoishia hapo walipo, namna mtu huyu anavyomfahamu mwenyeji wake, kuhusu kazi ya mtu fulani au kampuni iliyomuajiri au kuhusu mafunzo fulani.

5 Eleza jambo kuhusu wewe mwenyewe. Simulia hadithi yako mwenyewe; chagua mada ambayo inawafurahisha nyote.

6 Mueleze mwenzako kitu ambacho unahitaji kujua. Uliza swali la ukweli katika namna nzuri.

7 Tabasamu. Utakapotabasamu, watu wengi watakuwa huru kuzungumza na wewe. Mazungumzo mazuri huanza na tabasamu kidogo.

8 Hakikisha mnatazamana machoni.

# KARATASI YA ZOEZI 4.21

- Tazamana usoni na mtu ambaye unataka kuanzisha mazungumzo naye.
- Utakapokuwa makini na mtu, atafurahia hilo. Tambua kuwa hili halitokei mara nyingi.
- Unaweza kuzungumzia nini? Kwanza: zungumza kuhusu vitu ambavyo mnafanana, kwa mfano hali ya hewa ya kuvutia, ilhali kwamba mko kwenye mstari mmoja mbele yake n.k. mambo mengine yenye mfanano ni: marafiki wa aina moja ('Imekuwaje unamfahamu Fatuma'), matatizo ya aina moja (Je, na wewe pia unakosa umeme kwamba mara nyingi.......) mahali pa kufanana ('Ni mahali pazuri sana hapa, kweli?') malengo sawa ('Inapendeza sana! Nilikuwa pale pia').
- Zungumza uweze kumfahamu mwenzako, haijalishi mada ni ya kipuuzi kiasi gani.
- Ujanja ni kumuacha mwenzako azungumze. Hasa hasa kama hujui kitu cha kuongelea.
- Unampa nafasi mwenzako yakuzungumza kwa kuuliza maswali. Watu wanapenda sana kuongea, hasa hasa kuhusu wao binafsi.
- Usikilizaji makini mara nyingi ni bora kuliko kuongea. Utajifunza mengi kwa hilo na utapata marafiki kwa kusikiliza.
- Endelea kuuliza na kusikiliza. Kabla hujalijua hilo, una mazungumzo mazuri na umeshaanza kumfahamu mwenzako taratibu.
- Usibadilishe mazungumzo kuwa mahojiano. Endapo mwenzako anapenda kuongea, muache aongee na usikilize.

# JINSI YA KUWA KINARA KATIKA 'MAZUNGUMZO MAFUPI'? MADA YA 4.21

- Mazungumzo mengi huwa sio dayalojia. Mara nyingi inatokea kwamba watu wawili wanasubiri zamu ya kuzungumza. Hii haipendezi na haina uhalisia.
- Jenga tabia ya kujitambulisha.
- Unapompa mkono mwenzako mtazame machoni.
- Fahamu kuwa utakosea. Ila usihofu; watu husahau haraka.
- Usikose bashasha kabisa. Jicheke pale utakapozungumza kitu cha kushangaza.
- Kuwa muwazi na mwaminifu. Hii inafanya kazi vizuri sana. Usijifanye bora zaidi ya vile ulivyo.
- Fahamu kuwa watu wengi wangependa kuwa na mawasiliano zaidi na watu wanaowazunguka. Hii ina thamani sana kwa marafiki zako, familia yako na watu baki mtaani. Kila mtu anapenda tabasamu, 'habari ya asubuhi' yenye bashasha, mazungumzo mafupi ya kufurahisha, kila mtu anapenda pale mwenzakeanapomuonesha kuvutiwa nae.
- Mazungumzo mafupi ni muhimu sana. Huwa ni mwanzo wa jambo zuri kabisa. Vile utakavyozidi kuwa bora kwenye mahusiano na wengine, ndio maisha yako yatazidi kuwa bora. Utakutana na watu ambao mtaendana sana; utajifunza fikra mpya; utakuwa na maisha ya furaha na watu na utakuwa na mtandao salama wenye nguvu.